OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, MASUALA YA BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU

# MFUKO WA FIDIA KWA WAFANYAKAZI

# MPANGO MKAKATI

## 2022/23-2026/27



NOVEMBA 2021

OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, MASUALA YA BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU

# MFUKO WA FIDIA KWA WAFANYAKAZI

# MPANGO MKAKATI
## 2022/23-2026/27

NOVEMBA 2021

Yaliyomo

JEDWALI LA TOLEO LA NYARAKA ........ v
VIFUPISHO ........ vi
TAFSIRI ........ ix
DIBAJI ........ x
MUHTASARI ........ xi

**SURA YA KWANZA ........ 1**

**1.0 UTANGULIZI ........ 1**
1.1 Muktadha wa Mpango Mkakati ........ 1
1.2 Uanzishwaji wa Mfuko ........ 2
1.3 Majukumu ya Mfuko ........ 2
1.4 Kazi za Mfuko ........ 2
1.5 Dhima ........ 3
1.6 Dira ........ 3
1.7 Tunu ........ 3
1.8 Muundo wa Mpango ........ 3

**SURA YA PILI ........ 4**

**2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO MKAKATI WA KWANZA 2017/18-2021/22 KWA KIPINDI KILICHOISHIA TAREHE 30 JUNI 2021 ........ 4**
2.1 MAZINGIRA YA UENDESHAJI ........ 4
2.1.1 Viashiria vya Kiuchumi ........ 4
2.1.2 Ukuaji wa Pato la Taifa ........ 4
2.1.3 Kiwango cha Mfumuko wa Bei ........ 4
2.1.4 Viwango vya Riba ........ 5
2.1.5 Viwango vya kubadilisha Fedha ........ 5
2.1.6 Maendeleo ya Masoko ya Mitaji ........ 5
2.1.7 Utendaji wa Kiuchumi Kikanda ........ 6
2.1.8 Masuala Muhimu Kutokana na Mazingira ya Uendeshaji ........ 6
2.2 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MALENGO YA KIMKAKATI ........ 6
2.2.1 Boresha Taswira ya Mfuko ........ 7
2.3 Mtazamo wa Kifedha ........ 8
2.3.1 Kuboresha Uwezo wa Kifedha ........ 8
2.4 Mtazamo wa Ndani wa Mfumo wa Utendaji Kazi ........ 13
2.4.1 Kuongeza wigo wa Wanachama ........ 13
2.4.2 Kuboresha Ufanisi wa Uendeshaji ........ 15
2.4.3 Ukadiriaji wa Uzingatiaji wa Kitaasisi ........ 20
2.4.4 Kukuza Afya na Usalama Mahali pa Kazi ........ 21
2.4.5 Kuboresha Usimamizi wa Uhusiano na Washirika ........ 22
2.5 Mtazamo wa Kujifunza na Ukuaji ........ 22

| | | |
|---|---|---|
| 2.5.1 | Kuimarisha Utawala | 23 |
| 2.5.2 | Kuboresha Ujuzi na Maarifa kwa Wafanyakazi | 24 |
| 2.5.3 | Kuboresha Mazingira na Utamaduni wa Kazi | 25 |
| 2.6 | MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MSINGI | 26 |
| 2.7 | MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO 2016-2021 | 33 |
| 2.7.1 | Kujenga Msingi wa Kuigeuza Tanzania kuwa Taifa la Uchumi wa Kati wa Kiviwanda ifikapo 2025 | 33 |
| 2.7.2 | Kuboresha ubora wa maisha na ustawi wa binadamu | 33 |
| 2.7.3 | Kuhakikisha Mikataba ya Kimataifa na Kikanda Inatekelezwa kwa manufaa ya nchi | 34 |
| 2.8 | MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA CHAMA TAWALA 2015-2020 NA DIRA YA MAENDELEO YA TAIFA 2025 | 35 |
| 2.8.1 | Maisha Bora na Mapambano dhidi ya Umaskini | 35 |
| 2.8.2 | Utoaji wa Huduma Bora | 35 |
| 2.8.3 | Kuidhinishwa kwa Mikataba husika | 35 |
| 2.8.4 | Ulinzi wa Wafanyakazi | 35 |
| 2.8.5 | Mapambano dhidi ya Ufisadi | 35 |
| 2.8.6 | Maendeleo ya Viwanda | 36 |
| 2.8.7 | Utawala Bora | 36 |
| 2.9 | UCHAMBUZI WA HALI | 36 |
| 2.10 | Uwiano wa Malengo ya Kitaifa na Mkakati wa Mfuko | 36 |
| 2.11 | Hifadhi ya Jamii Tanzania Bara | 37 |
| 2.12 | Tathmini ya Mazingira | 38 |
| 2.12.1 | Viwezeshi (Uwezo na Fursa) | 38 |
| 2.12.2 | Changamoto (Mapungufu na Vihatarishi) | 38 |
| 2.12.3 | Wateja na Wadau | 38 |
| 2.12.4 | Pendekezo la Thamani ya Mteja | 39 |
| 2.13 | USIMAMIZI WA VIHATARISHI | 39 |
| 2.13.1 | Uchambuzi wa Vihatarishi | 39 |
| **SURA YA TATU** | | **45** |
| **3.0** | **MKAKATI WA MFUKO** | **45** |
| 3.1 | Pendekezo la Thamani ya Mteja | 45 |
| 3.2 | Maeneo ya Vipaumbele | 45 |
| 3.3 | Maeneo Makuu na Matokeo ya Kimkakati ya Mfuko | 47 |
| 3.4 | Mitazamo | 47 |
| 3.5 | Malengo Mkakati | 48 |
| 3.5.1 | Malengo Mkakati, Maelezo na Matokeo Tarajiwa | 48 |
| 3.6 | Ramani Mkakati | 51 |
| 3.7 | Ahadi ya Mfuko katika kutoa tija kwa Wadau | 51 |
| 3.8 | Vipimo vya Utendaji | 52 |

3.8.1 Vipimo vya Utekelezaji wa Malengo Mkakati ........ 52
3.9 Shughuli Mkakati ........ 53
3.10 Upimaji wa Malengo ya Mpango Mkakati wa Mfuko ........ 55

**SURA YA NNE ........ 59**

**4.0 MPANGO WA KIFEDHA ........ 59**
4.1 Utangulizi ........ 59
4.2 Nadharia za kiuchumi ........ 59
4.3 Vyanzo vya Mapato ........ 60
4.4 Matumizi ya Mapato ........ 60
4.5 Makadirio ya Kifedha ........ 61

**SURA YA TANO ........ 63**

**5.0 UFUATILIAJI WA MPANGO, TATHMINI NA UWAJIBIKAJI ........ 63**
5.1 Ufuatiliaji na Tathmini ........ 63
5.1.1 Uwajibikaji ........ 63
5.1.2 Kurugenzi inayohusika na Mipango ........ 63
5.1.3 Msimamizi wa Lengo ........ 64
5.1.4 Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ........ 64
5.1.5 Menejimenti ........ 64
5.1.6 Bodi ya Wadhamini ........ 64
5.1.7 Mapitio ya Mpango Mkakati ........ 64

**Kiambatisho: MPANGO WA UTEKELEZAJI ........ 66**
1.0 LENGO: KUONGEZA KIWANGO CHA KURIDHIKA KWA WANACHAMA NA WADAU ........ 66
2.0 LENGO: IMARISHA UWEZO ENDELEVU WA KIFEDHA ........ 69
3.0 LENGO: BORESHA UFANISI KATIKA UTENDAJI ........ 72
MMILIKI WA LENGO: DO ........ 72
4.0 LENGO: IMARISHA UZINGATIAJI ........ 73
MMILIKI WA LENGO: DO ........ 73
5.0 LENGO: IMARISHA UTAWALA ........ 75
MMILIKI WA LENGO: HLSU ........ 75
6.0 LENGO: BORESHA TEKNOLOJIA ........ 77
MMILIKI WA LENGO: HICTU ........ 77
7.0 LENGO: IMARISHA UWEZO WA WATUMISHI ........ 78
MMILIKI WA LENGO: HHRMAU ........ 78
Kiambatisho 3: TATHMINI YA WADAU ........ 81

# JEDWALI LA TOLEO LA NYARAKA

| | |
|---|---|
| Taasisi | MFUKO WA FIDIA KWA WAFANYAKAZI |
| Nyaraka | MPANGO MKAKATI 2022/23-2026/27 |
| Toleo Msingi | 2017 |
| Muda wa marejeo | Miaka miwili na nusu |
| Mpango wa sasa | 2021 |
| Namba ya toleo | Mpango Mkakati wa Kwanza |
| Inaratibiwa na | Mkurugenzi anayehusika na Masuala ya Mipango |
| Imependekezwa na | Menejimenti |
| Imeidhinishwa na | Bodi ya Wadhamini |

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **BCM** | Usimamizi wa Mwendelezo wa Shughuli za Taasisi |
| **BOT** | Benki Kuu ya Tanzania |
| **BRELA** | Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni |
| **BSC** | Mfumo wa Kupanga Matokeo |
| **CSR** | Wajibu wa Shirika kwa Jamii |
| **DFPI** | Mkurugenzi wa Fedha, Mipango na Uwekezaji |
| **DAS** | Mkurugenzi wa Huduma za Tathmini |
| **DMS** | Mfumo wa Usimamizi wa Nyaraka |
| **DO** | Mkurugenzi wa Uendeshaji |
| **DRs** | Wakurugenzi |
| **e-GA** | Mamlaka ya Serikali Mtandao |
| **ECASSA** | Taasisi ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya Afrika Mashariki na Kati |
| **ERP** | Mpango wa Rasilimali wa Shirika/Taasisi |
| **GDP** | Pato la Taifa |
| **GN. No.** | Namba ya Gazeti la Serikali |
| **HASSRMU** | Mkuu wa kitengo cha Uthamini, Takwimu na Usimamizi wa Hadhari |
| **HCP** | Watoa Huduma za Afya |
| **HHRMAU** | Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi Rasilimali Watu na Utawala |
| **HIAU** | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani |
| **HICTU** | Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia, Habari na Mawasiliano |
| **VVU** | Virusi vya Ukimwi |
| **HLSU** | Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria |
| **HPMU** | Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi |
| **HPRU** | Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa Umma |
| **HoD** | Wakuu wa Idara |
| **HR** | Rasilimali Watu |
| **HSP** | Watoa Huduma za Afya |
| **ICT** | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **ILO** | Shirika la Kazi Duniani |

| | |
|---|---|
| **IoDT** | Taasisi ya Wakurugenzi Tanzania |
| **ISO** | Shirika la Viwango la Kimataifa |
| **ISSA** | Taasisi ya Kimataifa ya Sekta ya Hifadhi ya Jamii |
| **LATRA** | Mamlaka ya usafiri wa Nchi Kavu |
| **LSU** | Kitengo cha Huduma za Sheria |
| **LTPP** | Mpango wa Kimtazamo wa Muda Mrefu |
| **M&E** | Ufuatiliaji na Tathmini |
| **MAC** | Mfumo wa Usimamizi wa Madai ya Wanachama |
| **MITI** | Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji |
| **MoFP** | Wizara ya Fedha na Mipango |
| **MoH** | Wizara ya Afya |
| **MoHA** | Wizara ya mambo ya Ndani |
| **MOAT** | Chama cha Wanahabari Tanzania |
| **MoU** | Mkataba wa Makubaliano |
| **MTEF** | Mfumo wa Matumizi wa Muda wa Kati |
| **MTSPBM** | Miongozo ya Mkakati wa Mipango ya Muda wa Kati |
| **MUM** | Mpango wa Ununuzi wa Mwaka |
| **NBS** | Idara ya Takwimu ya Taifa |
| **NFYDP** | Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano |
| **NIDA** | Mamlaka ya Taifa ya Vitambulisho |
| **OSH/AUMK** | Afya na Usalama Mahali pa Kazi |
| **OTR** | Ofisi ya Msajili wa Hazina |
| **OSHA** | Mamlaka ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi |
| **PMO-LYED** | Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Masuala ya Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu |
| **PO-PSM** | Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi |
| **MKUU** | Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma |
| **PRU** | Kitengo cha Uhusiano wa Umma |
| **R.E.** | Toleo Rejea |

| | |
|---|---|
| **ROI** | Mapato ya Uwekezaji |
| **SLA** | Mkataba wa Huduma kwa Mteja |
| **SWOC** | Uwezo, Mapungufu, Fursa na Changamoto |
| **TDV** | Dira ya Maendeleo ya Taifa Tanzania 2025 |
| **TIRA** | Mamlaka ya Udhibiti wa Bima Tanzania |
| **TMF** | Jumuiya ya Wanahabari Tanzania |
| **TNA** | Tathmini ya Mahitaji ya Mafunzo |
| **TRA** | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| **TEHAMA** | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **TSSA** | Taasisi ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii Tanzania |
| **Shilingi** | Shilingi ya Tanzania |
| **URT** | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| **UMFC** | Uwezo, Mapungufu, Fursa na Changamoto |
| **WCF** | Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi |

# TAFSIRI

| NENO | Maana |
|---|---|
| Sheria | Sheria ya Fidia Kwa Wafanyakazi [Sura ya 263] |
| Mfuko | Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi |
| Wateja | Wateja ni wanufaika wa moja kwa moja wa huduma au bidhaa za taasisi. Wateja wetu ni pamoja na waajiriwa, wategemezi wao na waajiri. |
| Vipimo vya Utendaji | Kipimo cha utendaji kinachotoa uthibitisho halisi wa kupiga hatua kuelekea lengo mkakati. |
| Wadau | Hujumuisha watu, vikundi, na taasisi zenye maslahi katika Mfuko, mfano wateja, watoa huduma, wadhibiti, wakurugenzi, waleta huduma, na makundi ya kijamii. |
| Shughuli Mkakati | Mradi au Jambo muhimu litakaloboresha utendaji katika lengo |
| Malengo Mkakati | Shughuli endelevu za uboreshaji, zinazowianishwa katika mitazamo, ambazo zinagawa mkakati katika kazi ndogondogo na kuwezesha mkakati kufanyika ukihusisha wafanyakazi wote katika kutekeleza malengo ya taasisi |
| Tokeo Mkakati | Matokeo ya mwisho yatokanayo na mafanikio ya utekelezaji wa mkakati wa taasisi. |
| Dhima Mkakati | Maeneo matatu au manne ya msisitizo wa mkakati yanayotambulisha mkakati mkuu wa kiutendaji katika taasisi, yakibainisha dira na lengo kuu katika vitendo, na kuwekeza nguvu katika matokeo mkakati yanayotarajiwa |
| Picha Mkakati | Ni mahusiano ya visababishi na matokeo yake baina ya malengo katika mitazamo minne. Malengo yenye muunganiko huonesha jinsi taasisi inavyolenga kutoa huduma bora. |
| Mkakati | Maamuzi ya Kimkakati yaliyofanywa, hatua zilizochukuliwa, kutokana na maamuzi na vitendo mbalimbali vinavyowezekana katika kuisaidia taasisi kutoka katika hali iliyopo kuelekea hali inayokusudiwa ili kufikia dira ya taasisi. |
| Shabaha | Utekelezaji katika kiwango tarajiwa kwa kipindi husika. |
| Dira | Taswira ya baadaye inayoamsha hisia ambayo taasisi inatarajia kuifikia. |

# DIBAJI

Kwa niaba ya Bodi ya Wadhamini, nafurahi kuwasilisha Mpango Mkakati wa pili wa Mfuko. Mpango Mkakati huu unalenga kutoa mwelekeo wa utekelezaji wa kazi za taasisi yetu hadi kufikia Juni 30, 2027. Mikakati iliyoainishwa katika mpango huu inalenga kufikia dira ya Mfuko yakuwa "mfano wa kuigwa katika utoaji wa huduma za fidia kwa wafanyakazi barani Afrika". Aidha, Mpango huu unategemea kukidhi matarajio ya Serikali na ya wadau wengine ya kutoa fidia stahiki na toshelevu kwa wakati kwa wafanyakazi wanaopata ajali au magonjwa yatokanayo na kazi na kwa wategemezi pale mfanyakazi anapofariki dunia.

Wakati wa utekelezaji wa Mpango Mkakati wa 2017/18-2021/22, Mfuko ulipata mafanikio mbalimbali ikiwa ni pamoja na mambo ya kujifunza. Katika kutekeleza majukumu yake, Mfuko uliweka mfumo madhubuti wa utoaji huduma ya malipo ya fidia wa kidijiti ambapo jumla ya shilingi bilioni 30.62 zililipwa kwa wanufaika mbalimbali. Fidia zinazolipwa zinakidhi viwango vinavyopendekezwa na Shirika la Kazi Duniani (ILO) vya asilimia 60 ya kipato halisi cha mfanyakazi bila kuathiri uendelevu wa Mfuko. Katika kutathmini hali ya kifedha, Mfuko ulifanya tathmini ya uhai na uendelevu na ilionesha kuwa Mfuko upo imara kifedha na kwa kipindi cha makadirio cha miaka thelathini (30) kinachoishia mwaka 2048.

Mfuko umeandaa Mpango Mkakati mpya kwa kushirikisha wadau wa ndani ikijumuisha Kurugenzi na Vitengo vyote pamoja na wadau wa nje. Mapendekezo ya wadau yalikusanywa na kuchambuliwa kupitia utafiti uliofanywa kati ya mwezi Julai na Septemba 2021 na kuzingatiwa katika uandaaji wa Mpango Mkakati. Kwa umuhimu huo huo, Mpango Mkakati umezingatia kikamilifu Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na uchumi wa viwanda kama kipaumbele cha maendeleo ya Taifa. Hivyo basi, tunaamini kwamba utekelezaji wa Mpango huu utaendelea kuuweka Mfuko katika mwelekeo sahihi.

Mwisho, napenda kuwahakikishia wadau juu ya dhamira yetu kama Bodi kutekeleza majukumu yetu kwa weledi na ufanisi kwa maslahi mapana ya wanachama, Serikali na wadau wengine. Bila shaka, tutakutana na changamoto katika utekelezaji wa mpango huu. Hata hivyo, kwa kupitia ushirikiano na mashauriano na wadau muhimu, hatuna shaka kwamba Mfuko utazikabili changamoto hizo na kufikia malengo yake.



Bw. Emanuel B. Humba
**MWENYEKITI WA BODI**

# MUHTASARI

Mfuko umeanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi [Sura 263]. Uanzishwaji wa Mfuko ni matokeo ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2003 ambayo imeainisha maeneo yenye mapungufu katika sekta ya hifadhi ya jamii yanayohitaji serikali kutengeneza sera ya kukabili mapungufu hayo. Baadhi ya mapungufu yaliyoainishwa katika Sera hiyo ni pamoja na kundi kubwa la wananchi kutofikiwa na mfumo rasmi wa hifadhi ya jamii, ufinyu wa fidia inayolipwa na kukosekana kwa uratibu wa pamoja katika sekta. Kutungwa kwa Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi [Sura ya 263] kulifuta Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi ya mwaka 1949 ili kuhakikisha kuwa wafanyakazi wa sekta binafsi na umma Tanzania Bara wanalipwa fidia stahiki.

Utaratibu wa ulipaji ya fidia kabla ya kuanzishwa kwa sheria ya sasa ulikosa ufanisi na ulishindwa kujibu changamoto zilizoikabili nguvukazi. Baadhi ya mapungufu ni pamoja na ufinyu wa fidia iliyokuwa ikilipwa, malipo kufanywa kwa njia ya mkupuo badala ya pensheni pamoja na urasimu uliokuwepo katika mfumo wa malipo. Mapungufu haya yalilazimisha kuanzishwa kwa Mfuko kwa lengo la kutoa suluhisho la changamoto zilizowakabili wafanyakazi ikiwa ni pamoja na kuboresha utoshelevu wa fidia inayolipwa kwa wafanyakazi wanaopata ajali, magonjwa au kufariki wakati wakitekeleza majukumu yao ya kikazi.

Dhima ya Mfuko ni ““Kutoa Huduma za Fidia za Kuaminika na Fanisi kwa Wafanyakazi zitakazowawezesha kukabiliana na Athari za Kijamii na Kiuchumi zitokanazo na kuumia kazini”. Pamoja na dhima hii, dira ya Mfuko ni “Mfano wa kuigwa katika utoaji wa huduma za fidia kwa wafanyakazi barani Afrika”.

Katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa Mpango huu, Mfuko utajikita katika maeneo sita ya kipaumbele ambayo ni; kuimarisha mtandao wa ofisi za Mfuko, kuendeleza rasilimali watu, kufanya uwekezaji kwa umakini, kukuza ukusanyaji wa michango, kuwekeza katika teknolojia ya kisasa na kuboresha huduma. Malengo Mkakati saba (7), yaliyoibuliwa kutoka katika dhamira Mkakati nne (4), yamepangwa kutekelezwa katika kipindi hicho ili kufanikisha majukumu ya Mfuko.

Aidha, katika jitihada ya kuhakikisha kuwa malengo haya yanatekelezwa kikamilifu, bajeti ya Mfuko ya kila mwaka pamoja na shughuli zitakazotekelezwa zitazingatia Mpango Mkakati huu. Tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mpango itafanyika mara kwa mara kwa lengo la kupima kama malengo yanafikiwa na pale inapobidi, kuchukua hatua stahiki.

Mapitio ya Mpango yatafanyika baada ya miaka miwili na nusu ya utekelezaji au wakati wowote itakapohitajika kulingana na mabadiliko ya utendaji kazi hasa katika mazingira ya nje ya taasisi.

Dkt. John K. Mduma

**MKURUGENZI MKUU**

WCF

Workers Compensation Fund

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Muktadha wa Mpango Mkakati

Mpango Mkakati huu umeandaliwa kwa kushirikisha wadau wa ndani yaani Kurugenzi na Vitengo vyote pamoja na wadau wengine. Mpango huu umeandaliwa kwa kufuata nadharia ya ''Balanced Scorecard'' (BSC) inayoweka vipaumbele katika mitazamo minne. Nadharia ya BSC inatazama taasisi katika mtazamo wa wateja, mtazamo wa usimamizi wa fedha, mtazamo wa mifumo ya ndani ya utendaji kazi na mtazamo wa kujifunza na ukuaji.

Mtazamo wa wateja unalenga kuwaangalia wadau wanaonufaika na huduma za Mfuko. Mfuko unautambua mtazamo wa wateja kama kipaumbele cha kwanza katika mitazamo yote minne kwa kuhakikisha thamani kwa mteja inaboreshwa kwa kuweka njia rafiki za kutolea huduma kwa gharama nafuu. Mtazamo wa kifedha unalenga kuhakikisha kuwa Mfuko una uwezo wa kifedha wakati wote kwa lengo la kufikia matarajio ya wadau wake. Mtazamo wa mifumo ya ndani ya utendaji kazi unalenga kuangalia ufanisi wa taratibu na mifumo ya utendaji kazi. Lengo la mtazamo huu ni kuhakikisha uwepo wa uwazi na ufanisi katika kutoa huduma. Mtazamo wa Kujifunza na Ukuaji unalenga kuangalia jinsi wafanyakazi watakavyojengewa uwezo kwa kupewa mafunzo, stadi na ujuzi kwa lengo la kuongeza ufanisi na kufikia malengo ya Mfuko, kujenga uwezo wa taasisi na kuboresha matumizi ya kidijiti. Katika kipindi cha Mpango huu, mafunzo mbalimbali katika maeneo ya vipaumbele yatatolewa kwa wafanyakazi kwa lengo la kuwaongezea ujuzi.

Mfuko utazingatia utekelezaji wa lengo lake kuu la kulipa fidia kwa wafanyakazi waliopata ulemavu kutokana na ajali au magonjwa yanayotokana na kazi na kwa wategemezi wao iwapo watafariki. Katika kufikia lengo hili, Mpango utazingatia nguzo nne ambazo ni ufanisi katika uendeshaji, ustahimilivu wa kifedha, kujali mteja na ushirikiano wa kimkakati.

Utekelezaji wa Mpango Mkakati huu unategemewa kuchangia katika kufikiwa kwa Malengo ya Taifa kupitia kuhamasisha tija ya nguvukazi, kuzuia ajali na magonjwa mahali pa kazi, programu za kuwawezesha wafanyakazi walioumia kurejea kazini na kutoa fidia kwa wafanyakazi waliopata ulemavu au kufariki kutokana na ajali au magonjwa yanayotokana na kazi na hivyo kuongeza pato la taifa, ajira na kipato cha wananchi.

Mfumo madhubuti wa upangaji mikakati na usimamizi wa utendaji kazi unaoakisi dhana ya Balance Scorecard umetumika kuoanisha dira ya Mfuko inayoshirikisha shughuli mkakati, mwenendo tegemewa wa wafanyakazi pamoja na utendaji wa kila siku wa Mfuko. Vipimo vya utekelezaji wa Mkakati vilisaidia kuboresha ufanyaji maamuzi na kuonyesha hatua iliyofikiwa katika kupata matokeo tarajiwa. Hii itawezesha Mfuko kujikita katika masuala ya msingi yanayohitajika kufikia dira na matarajio ya wananchi, wadau na wafanyakazi wake. Manufaa mengine yanayotarajiwa ni pamoja na uboreshaji wa vipaumbele, mawasiliano ya ndani na ya nje na kuwepo kwa muunganiko kati ya makadirio ya matumizi na michakato na mkakati wa usimamizi wa gharama.

## 1.2 Uanzishwaji wa Mfuko

Mfuko ulianzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 5 cha Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi [Sura 263]. Lengo kuu la kuanzishwa kwa Mfuko ni kutoa fidia stahiki na toshelevu kwa wafanyakazi ambao watapata ajali au magonjwa yatokanayo na kazi na ikiwa ni kifo, fidia italipwa kwa wategemezi wao.

Kutungwa kwa Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi kulipelekea kufutwa kwa Sheria ya zamani ya Fidia kwa Wafanyakazi ya mwaka 1949 na kufanyika kwa marekebisho katika Kifungu cha 33 cha Sheria ya Utumishi wa Umma [Sura 298] pamoja na Kanuni Na. 111 na 112 za Sheria ya Utumishi wa Umma za mwaka 2003.

Mfuko ulianza rasmi shughuli zake tarehe 1 Julai 2015 kufuatia Tangazo za Serikali Na. 169 la tarehe 1 Mei 2015. Mfuko ulipewa kipindi cha mwaka mmoja hadi tarehe 30 Juni 2016 kabla ya kuanza kulipa fidia. Kazi zilizoanza kutekelezwa na Mfuko tarehe 1 Julai 2015 ni pamoja na usajili wa waajiri, ukusanyaji wa michango, uwekezaji na utoaji wa mafunzo kwa wadau.

Kuhusu viwango vya uchangiaji na ulipaji mafao, Waziri mwenye dhamana hutangaza viwango husika kabla ya kuanza kwa mwaka mpya wa fedha. Aidha kwa sasa waajiri wote katika sekta za umma na binafsi Tanzania Bara wanahitajika kuchangia kiwango cha asilimia 0.5 na 0.6 ya mapato ya jumla mtawalia.

## 1.3 Majukumu ya Mfuko

Majukumu ya Mfuko yanatokana na malengo makuu ambayo ni:

- (a) Kulipa fidia stahiki na toshelevu kwa wafanyakazi;
- (b) Kutekeleza Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2003;
- (c) Kutekeleza matakwa ya Kifungu cha 5 cha Sheria,
- (d) Kuweka utaratibu utakaowezesha kuharakisha malipo ya fidia kwa wafanyakazi na wategemezi wao;
- (e) Kuweka mfumo wa udhibiti na usimamizi wa michango na malipo ya fidia;
- (f) Kuimarisha kinga za ajali na magonjwa mahali pa kazi;
- (g) Kutoa huduma za utengemao;
- (h) Kutekeleza matakwa ya mikataba ya kimataifa inayohusu fidia kwa wafanyakazi.

## 1.4 Kazi za Mfuko

Kazi za Mfuko ni:

- (a) Kulipa fidia kwa wafanyakazi;
- (b) Kukusanya michango kutoka kwa waajiri;
- (c) Kuwekeza fedha za ziada;
- (d) Kusajili waajiri wote Tanzania Bara;
- (e) Kutathimini mazingira hatarishi mahali pa kazi na viwango vya gharama;
- (f) Kutunza kumbukumbu za matukio ya ajali kazini, magonjwa na vifo;
- (g) Kukuza mbinu za kuzuia ajali, magonjwa na vifo vitokanavyo na kazi;
- (h) Kufanya programu za kutoa elimu ya uelewa kwa umma.

## 1.5 Dhima

“Kutoa Huduma za Fidia za Kuaminika na Fanisi kwa Wafanyakazi zitakazowawezesha kukabiliana na Athari za Kijamii na Kiuchumi zitokanazo na ajali mahali pa kazi”

## 1.6 Dira

“Mfano wa Kuigwa katika Utoaji wa Huduma za Fidia kwa Wafanyakazi barani Afrika”

## 1.7 Tunu

Mfuko unaongozwa na tunu tano ambazo zinaongoza mienendo ya wafanyakazi na utekelezaji wa majukumu yao. Tunu hizi zinashawishi utamaduni wa Mfuko na namna ambavyo maamuzi hufanyika. Jedwali Na.1 linaelezea imani ya Mfuko, jinsi tunu zilivyo na mchango katika kufikia dira ya Mfuko.

Uadilifu, Ushirikiano, Uwajibikaji, Ubora na Kujali ndiyo mizizi ya misingi mikuu ya Mfuko. Msingi hii itaendelea kuthaminiwa na ndio itaongoza matendo na mahusiano. Maelezo ya kina kwa kila tunu yapo kwenye Jedwali Na. 1 hapa chini.

**Jedwali Na. 1: Maelezo ya Tunu Msingi**

| Na | Tunu | Maelezo |
|---|---|---|
| **1** | Uadilifu | Siku zote tutakuwa waaminifu na wenye maadili, tukidumisha utawala bora na kuwa wawazi katika kutoa taarifa wanazostahili kwa wadau wetu |
| **2** | Ushirikiano | Tunaamini katika ushirikiano wenye lengo la kubadilishana ujuzi, maarifa na uzoefu ili kufanikisha malengo muhimu ya Mfuko na kuendeleza ushirikiano kati ya watumishi na wadau. |
| **3** | Uwajibikaji | Tutawajibika kwa yote tufanyayo katika ngazi ya taasisi na ya mfanyakazi binafsi na kutoa majawabu stahiki kwa hoja za wadau wetu. |
| **4** | Ubora | Tutajenga uwezo, mazingira wezeshi na miundombinu rafiki ya kutoa huduma bora zinazozidi matarajio ya wateja. |
| **5** | Kujali | Tutawahudumia wateja wetu kwa upendo, uadilifu na utaalamu wa hali ya juu. |

## 1.8 Muundo wa Mpango

Mpango Mkakati huu umegawanyika katika sura tano (5). Sura ya Kwanza inaeleza utangulizi unaojumuisha historia ya Mfuko, dhamana, kazi na majukumu, mbinu, lengo na mpangilio. Sura ya Pili inaelezea Mapitio ya Utendaji kazi wa Mfuko kwa kipindi cha miaka mitano ya Mpango Mkakati wa kwanza (2017/18 -2021/22), tathmini ya wadau, uchambuzi wa mazingira ya ndani na nje kwa kutumia uainishaji wa Uwezo, Mapungufu, Fursa na Changamoto (SWOC), Usimamizi wa Vihatarishi na matarajio ya Wadau. Sehemu ya Tatu inajumuisha Dira, Dhima, Tunu Msingi, Malengo Mkakati, Vipimio vya Utendaji, shabaha na jitihada za kushughulikia mambo mbalimbali.

Sura ya Nne inaeleza mipango ya kifedha kwa kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa Mpango Mkakati huu. Sura ya Tano inatoa mwongozo kuhusu Ufuatiliaji wa Mpango, Tathmini na Utoaji wa Taarifa ya utekelezaji.

# SURA YA PILI

## 2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO MKAKATI WA KWANZA 2017/18-2021/22 KWA KIPINDI KILICHOISHIA TAREHE 30 JUNI 2021

## 2.1 MAZINGIRA YA UENDESHAJI

### Utangulizi

Sura hii inaonesha viashiria vya kiuchumi na kijamii katika kipindi cha kuanzia Julai 2017 hadi Juni 2021.

#### 2.1.1 Viashiria vya Kiuchumi

#### 2.1.2 Ukuaji wa Pato la Taifa[1]

Ukuaji wa Pato la Taifa huashiria kiwango cha tija katika uzalishaji pamoja na uwepo wa ajira katika uchumi. Uzalishaji wenye tija kwenye biashara na uwepo wa ajira katika uchumi unaleta matokeo chanya kwa Mfuko kupitia usajili na ukusanyaji wa michango kutoka kwa waajiri. Hivyo, ukuaji mzuri wa uchumi ni nguzo katika uendelevu wa Mfuko. Katika kipindi cha mapitio, kiwango cha ukuaji wa uchumi ni asilimia 6.9 kwa mwaka 2017 na kuongezeka hadi asilimia 7.0 kwa mwaka 2018. Hata hivyo katika mwaka 2019, kasi ya ukuaji wa pato la taifa ilibakia katika kiwango cha asilimia 7.0 wakati kasi ya ukuaji wa pato la taifa ikipungua hadi asilimia 4.8 kutokana na madhara ya janga la UVIKO-19. Kwa mujibu wa Wizara ya Fedha na Mipango, ukuaji wa pato la taifa unatarajiwa kuongezeka hadi kufikia asilimia 5.6 mwaka 2021 kutokana na juhudi zinazoendelea za kimataifa kuhusu chanjo na kuzuia UVIKO-19. Muhtasari wa viwango vya ukuaji wa pato la taifa katika kipindi husika ni kama inavyoonekana katika **Jedwali 1.**

**Jedwali 1:** Kiwango cha Ukuaji wa Uchumi

| Mwaka | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kiwango cha ukuaji | 6.8% | 6.9% | 7.0% | 7.0% | 4.8% | 5.6% |

#### 2.1.3 Kiwango cha Mfumuko wa Bei[2]

Mfumuko wa bei huathiri uwekezaji wa muda mfupi na mrefu wa Mfuko. Mfumuko wa bei wa wastani huweka mazingira rafiki kwa shughuli za uwekezaji. Hivyo Mfuko unatarajia kuwa na viwango vya wastani vya utendaji kazi katika shughuli za uwekezaji pamoja na utoshelevu wa mafao kwa wanufaika wake. Katika kipindi cha mapitio, mfumuko wa bei ulipungua kutoka asilimia 5.3 mwaka 2016/17 hadi asilimia 3.2 kwa mwaka 2020/21. Mfumuko wa bei kwa robo iliyoishia Septemba 2021 ulikuwa asilimia 4.0. Viwango vingine vya mfumuko wa

1 MOFP, National Economic Survey Book – September 2021
2 MOFP, National Economic Survey Book – September 2021

bei ni kama vinavyooneshwa katika **Jedwali la 2**.

**Jedwali la 2:** Wastani wa Viwango vya Mfumuko wa Bei kwa Mwaka

| Mwaka wa Fedha | 2016/17 | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mfumuko wa bei | 5.3% | 4.3% | 3.2% | 3.5% | 3.2% | 4.0% |

### 2.1.4 Viwango vya Riba[3]

Kiwango cha riba kilichopo katika soko la fedha kinaamua mapato ya uwekezaji. Ili kupata mapato mazuri, Mfuko huchagua maeneo ya uwekezaji yenye viwango vizuri vya riba. Katika kipindi husika, wastani wa riba iliyotumika na benki za kibiashara katika utoaji wa mikopo ulipungua kutoka asilimia 18.30 mwaka 2017 hadi 15.70 mwaka 2020, wakati riba ya kuweka akiba ilipungua kutoka asilimia 11.70 mwaka 2017 hadi 8.30 mwaka 2020. Viwango vya riba vimeoneshwa kwenye **Jedwali la 3** hapa chini.

**Jedwali la 3:** Viwango vya Riba

| Mwaka | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kiwango cha kukopesha kwa muda mfupi (miezi 12) | 13.70% | 18.30% | 18.20% | 16.70% | 15.70% |
| Kiwango cha riba ya akiba kwa muda mfupi (miezi 12) | 11.50% | 11.70% | 8.80% | 8.80% | 8.30% |
| Tofauti ya viwango vya riba | 2.19% | 6.64% | 9.47% | 7.89% | 7.45% |

### 2.1.5 Viwango vya kubadilisha Fedha[4]

Kiwango cha ubadilishaji fedha huathiri uuzaji na uingizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi pamoja na uingizaji wa mitaji ya kigeni katika uchumi. Viwango rafiki vya kubadilisha fedha huchochea tija katika ufanyaji biashara na kuongeza ajira. Hali hii husaidia katika kusajili waajiri na ukusanyaji wa michango. Katika kipindi cha mapitio, thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani ilishuka kutoka Shilingi 2,188.00 kwa Dola moja kwa mwaka 2016 hadi Shilingi 2,305.60 kwa mwaka 2020. Hivyo, gharama ya kuagiza bidhaa kutoka nje iliongezeka. Hata hivyo, uwepo wa matumizi kidogo ya fedha za kigeni kwa Mfuko unapunguza athari za moja kwa moja. Wastani wa viwango vya ubadilishaji wa fedha katika kipindi husika ni kama inavyoonekana katika **Jedwali la 4**.

**Jedwali la 4:** Wastani wa Viwango vya Ubadilishaji Fedha kwa Mwaka

| Mwaka | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
|---|---|---|---|---|---|
| Viwango vya kubadilisha fedha (Shilingi/USD) | 2,188.00 | 2,240.80 | 2,275.40 | 2,299.80 | 2,305.60 |

### 2.1.6 Maendeleo ya Masoko ya Mitaji [5]

Hali ya maendeleo ya Soko la Mitaji inaathiri Mfuko kupitia umiliki wa hisa katika taasisi na kampuni mbalimbali. Maendeleo chanya katika soko la mitaji huleta ufanisi katika uwekezaji. Katika kipindi husika, maendeleo ya Soko la mitaji la Dar es Salaam (DSE) yalipungua kwa

3 MOFP, National Economic Survey Book – September 2021

4 MOFP, National Economic Survey Book – September 2021

5 DSE, Market Report 31st July, 2016 and 31st December, 2020

asilimia 52.8 kutoka Shilingi bilioni 23,076.01 Desemba 2017 hadi Shilingi bilioni 15,095 Desemba 2020. Mabadiliko makubwa ya bei za hisa yalitokana na kupungua kwa uwekezaji katika Soko.

### 2.1.7 Utendaji wa Kiuchumi Kikanda [6]

Hali ya utendaji wa shirikisho la kiuchumi kikanda unategemea viashiria vya ukuaji wa uchumi kama vile viwango vya ubadilishaji fedha na uwiano wa malipo katika jumuiya mbalimbali za kikanda ambazo nchi husika ni mwanachama kama vile Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC). Uendeshaji mzuri wa shughuli za kiuchumi katika Nchi wanachama unaimarisha masuala ya uwekezaji, kuongeza tija katika uzalishaji na kuongeza wigo wa soko la ajira, na hivyo kunufaisha Mfuko kupitia usajili, ukusanyaji wa michango na uwekezaji. Katika kipindi husika, Jumuiya ya Afrika Mashariki ilikumbwa na kushuka kwa uwiano wa malipo kwa dola milioni 1,117.2 kwa mwezi Aprili 2020 na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa pato la taifa hadi asilimia 5.7 kwa mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 6.0 kwa mwaka 2019. Aidha, Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) ilikumbwa na kupungua kwa ukuaji wa uchumi hadi asilimia 2.0 kwa mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 3.5 kwa mwaka 2019.

### 2.1.8 Masuala Muhimu Kutokana na Mazingira ya Uendeshaji

Mapitio ya mazingira ya uendeshaji kwa kipindi cha miaka mitano yanaonyesha kuwa uchumi ulikuwa imara kwa miaka mitatu ya mwanzo. Katika mwaka 2020/21 uchumi ulishuka kutokana na janga la UVIKO-19. Hata hivyo makadirio ya mwaka 2021/22 yanaonyesha kuimarika kwa ukuaji. Hivyo, Mfuko unahitaji kuimarisha shughuli za utekelezaji kama vile usajili wa waajiri na ukusanyaji wa michango. Kadhalika, Mfuko unahitaji kuzingatia uwekezaji wenye tija ili kuimarisha uendelevu wa hali ya kifedha.

## 2.2 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MALENGO YA KIMKAKATI

Utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Mfuko kwa miaka mitano unatathminiwa kwa kuzingatia mitazamo minne. Kila mtazamo una malengo maalumu ambayo yaliwekwa ili kufikiwa. Mfuko ulifanya kazi chini ya malengo ya kimkakati kumi na moja (11). Hali ya utekelezaji wa kila lengo la kimkakati ni kama ifuatavyo.

#### 2.2.0.1 Mtazamo Unaomzingatia Mteja

Mtazamo unaomzingatia mteja unawalenga wadau wanaonufaika na huduma za Mfuko. Mfuko unachukulia mtazamo unaomzingatia mteja kama kipaumbele cha kwanza kati ya mitazamo mingine na kuhakikisha kuwa thamani ya mteja inaimarishwa kupitia upatikanaji wa huduma kwa gharama nafuu kadri iwezekanavyo na kwa kuboresha utoaji wa huduma. Mtazamo huu una malengo mawili ya kimkakati kama ifuatayo.

#### 2.2.0.2 Ongezeko la Kuridhika kwa Wateja

Lengo hili linakusudia kuhakikisha kuwa Mfuko unawathamini wateja wake kwa kutoa

6 National Statistic Office and IMF, World Economic Outlook, April 2020 and June 2020 updated

huduma zenye ubora wa hali ya juu na kwa uhakika, kwa wakati na kwa kutumia teknolojia inayofaa. Lengo hili hupimwa kwa kuangalia kiwango cha kuridhika kwa mteja.

#### 2.2.0.3 Kiwango cha Kuridhika kwa Wateja

Kiwango cha kuridhika kwa Wateja hupatikana kutokana na tafiti za kuridhika kwa wateja zinazofanywa kila mwaka. Katika kipindi cha mapitio, shabaha ya kiwango cha kuridhika kwa wateja ilikuwa ni asilimia 80 kufikia Juni 2022. Hali ya utekelezaji inaonyesha kuwa, kiwango cha kuridhika kwa wateja kimekuwa kikiongezeka kutoka asilimia 44.99 mwaka 2017/18, 51.60 mwaka 2018/19, 67.90 mwaka 2019/20 hadi 68.01 mwaka 2020/21 (**Kielelezo cha 1**). Kuongezeka huku kulitokana na juhudi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuandaa na kutekeleza Mpango wa Usimamizi wa Mahusiano na Wateja na utekelezaji wa Mkataba wa Huduma kwa Mteja.

Mfuko unakusudia kutekeleza hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na uboreshaji wa huduma kwa njia ya mtandao ili kupunguza muda unaotumika kushughulikia madai, uboreshaji wa mikakati ya kutoa elimu ya uelewa pamoja na utekelezaji mzuri wa makubaliano ya utoaji huduma ndani ya Mfuko. Utekelezaji wa hatua hizi unatarajiwa kuwezesha kupanda kwa kiwango cha kuridhika kwa wateja kufikia 80% ifikapo Juni 2022.

**Kielelezo cha 1:** Mwenendo wa Kiwango cha Kuridhika 2017/18-2021/22




### 2.2.1 Boresha Taswira ya Mfuko

Lengo hili linakusudia kuhakikisha kuwa wadau wanafahamu bidhaa na huduma za Mfuko. Lengo hili linapimwa kwa kiwango cha uelewa wa taswira ya taasisi.

#### 2.2.1.1 Kiwango cha Uelewa wa Taswira ya Taasisi

Kiwango cha uelewa wa taasisi hupatikana kutokana na tafiti za zinazofanywa kila mwaka. Lengo ni kubaini kwa kiasi gani huduma na mafao yanayotolewa yanajulikana na wadau.

Katika kipindi cha mapitio, shabaha ilikuwa kufikia kiwango cha uelewa kuhusu taasisi kwa asilimia 80 ifikapo Juni 2022.

Katika kipindi chote cha utekelezaji, kiwango cha taswira ya taasisi kimekuwa kikiongezeka hadi kufikia asilimia 74.94 Juni 2021 kutoka asilimia 64.20 mwaka 2017/18 **(Kielelezo Na. 2)**. Mafanikio hayo yamechangiwa na jitihada mbalimbali zilizofanywa na Mfuko ikiwa ni pamoja na kutumia vyombo vya habari katika utoaji wa elimu ya uelewa, utekelezaji wa Programu ya Marekebisho ya Uhamasishaji kuanzia 2020 ambayo ilisisitiza kampeni mahususi kwa mashirika ya umma, Jeshi la Polisi Tanzania na taratibu za malipo ya mafao kwa kushirikiana na Taasisi zingine za Umma zilizopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kama vile NSSF, PSSSF, Idara ya Kazi na OSHA. Utekelezaji wa hatua hizi pamoja na Mkakati wa Mawasiliano wa Taasisi unatarajiwa kuwezesha kiwango cha uelewa kufikia asilimia 80 ifikapo Juni 2022.

**Kielelezo cha 2:** Kiwango cha Mwenendo wa Jumla wa Uelewa wa Mfuko




## 2.3 Mtazamo wa Kifedha

Mtazamo huu unalenga kuhakikisha kwamba uendelevu wa kifedha wa Mfuko unaboreshwa wakati wote kutokana na umuhimu wake katika kukidhi matarajio ya wadau.

### 2.3.1 Kuboresha Uwezo wa Kifedha

Lengo hili linakusudia kuboresha ukuaji wa kifedha wa Mfuko ambao utauwezesha kutoa huduma za fidia kwa wafanyakazi katika hali endelevu. Lengo hili linapimwa kwa asilimia ya kiwango cha michango inayokusanywa dhidi ya lengo la mwaka, kiasi cha fedha kinachowekezwa dhidi ya jumla ya mapato yanayokusanywa, mapato yatokanayo na

uwekezaji, gharama za uendeshaji kwa uwiano wa jumla ya mapato pamoja na asilimia ya kubana matumizi.

#### 2.3.1.1 Asilimia ya Michango Iliyokusanywa dhidi ya Lengo la Bajeti

Michango ni chanzo kikuu cha mapato ya Mfuko na inakusanywa kutoka kwa waajiri wote wanaofanya shughuli zao Tanzania Bara. Michango inakokotolewa kulingana na pato ghafi la mfanyakazi lakini haikatwi kutoka kwenye mshahara wa mfanyakazi badala yake inalipwa na mwajiri. Katika kipindi cha mapitio, kiwango cha michango kilikuwa asilimia 0.5 na 1 kwa sekta ya Umma na Binafsi mtawalia kutoka 2015/16 hadi 2020/21 na asilimia 0.5 na 0.6 kwa Umma na Binafsi mtawalia mwaka 2021/22.

Lengo la Mfuko lilikuwa ni kukusanya asilimia 100 ya michango yote kila mwaka. Katika kipindi cha mapitio, wastani wa makusanyo ya michango ilikuwa Shilingi bilioni 84.08 sawa na asilimia 70.11 ya lengo. Hata hivyo, mwenendo wa uchangiaji ulikuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka: 2017/18 mchango halisi ulikuwa Shilingi bilioni 72.82, 2018/19 Shilingi bilioni 81.37, 2019/20 Shilingi bilioni 90.84, 2020/21 Shilingi bilioni 91.30 na mwaka 2021/22 makadirio ya makusanyo yanakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 91.46 (**Kielelezo cha 3**). Kutofikiwa kwa lengo kulisabishwa na baadhi ya waajiri kutochangia michango na kufungwa kwa biashara miongoni mwa waajiri kutokana na athari za UVIKO-19. Hata hivyo, ufanisi uliopatikana ulichangiwa na jitihada za Mfuko ikiwa ni pamoja na kufanya uhamasishaji kwa waajiri kuhusu masuala ya Fidia kwa Wafanyakazi, uwekaji wa mifumo inayojiendesha ya utendaji kazi katika usajili na uchangiaji, kufanya kaguzi za mara kwa mara na kaguzi zinazoshirikisha taasisi zingine.

Mfuko utaendelea kushirikiana na Taasisi mbalimbali za Umma na wadau wengine muhimu ili kuhakikisha waajiri wote ambao hawajasajiliwa wanatambulika, wamesajiliwa na wanachangia Mfuko.

**Kielelezo cha 3**: Mwenendo wa Makusanyo ya Michango



#### 2.3.1.2 Fedha Inayowekezwa Dhidi ya Mapato yote ya Mfuko kwa Mwaka

Mfuko unatakiwa kuwekeza mapato yote yanayobaki baada ya kutimiza matakwa ya uendeshaji kama vile malipo ya faida, gharama za usimamizi, matumizi ya mtaji, kodi ya shirika na gharama za usimamizi wa uwekezaji. Hivyo, Mfuko ulikadiria kuwekeza angalau asilimia 70 ya mapato yake yote ya kila mwaka. Katika kipindi cha mapitio, Mfuko uliwekeza asilimia 69.86 ya mapato yake yote ya Shilingi bilioni 480.95.

Katika mwaka 2017/18 Mfuko uliwekeza Shilingi bilioni 83.53, 2018/19 Shilingi bilioni 67.96, 2019/20 Shilingi bilioni 86.43, 2020/21 Shilingi bilioni 98.10 na mwaka 2021/22 Shilingi bilioni 137 zinatarajiwa kuwekezwa. Hali ya utekelezaji ilichangiwa zaidi na mabadiliko katika ukusanyaji wa michango ambayo ni chanzo kikuu cha mapato ya Mfuko. Hata hivyo, Mfuko ulifanikiwa kupata jumla ya Shilingi bilioni 226.19 kama faida kutokana na uwekezaji wa Shilingi bilioni 483.58.

Sababu kuu ya mafanikio ilitokana na jitihada za Mfuko kuwekeza fedha zilizopangwa kwenye vitega uchumi vyenye faida kubwa hasa dhamana za serikali.

Mfuko utaendelea kuchukua fursa za kuwekeza kwa wakati katika uwekezaji wa muda mrefu (Dhamana za Serikali) kwenye vitega uchumi vyenye tija ili kuwezesha kufikia uwiano wa asilimia 70 ya fedha zinazoweza kuwekezwa ukilinganisha na jumla mapato.

**Kielelezo cha 4**: Mwenendo wa Fedha Zinazoweza Kuwekezwa Kulinganisha na Jumla ya Mapato




#### 2.3.1.3 Mapato ya Uwekezaji

Miongozo ya udhibiti ya uwekezaji inahitaji kwamba angalau mapato halisi ya uwekezaji ya asiimia 1 yapatikane. Lengo la Mfuko katika kipindi cha mapitio lilikuwa angalau asilimia 3 ya mapato halisi yawe yamefikiwa kila mwaka. Asilimia ya mapato halisi ya uwekezaji hupatikana kwa kupunguza kiwango cha mfumuko wa bei kutoka kwenye mapato yaliyopatikana kwenye

uwekezaji. Katika kipindi cha mapitio, asilimia ya mapato ya uwekezaji imekuwa juu ya lengo katika kipindi chote cha mapitio (**Kielelezo cha 5**). Ufanisi huo ulichangiwa na uwekezaji wenye tija wa Mfuko na kiwango cha chini cha mfumuko wa bei. Matokeo yake, mapato ya jumla kutokana na uwekezaji katika kipindi cha mapitio yalikuwa Shilingi bilioni 132.46. Mfuko utaendelea kufanya uchambuzi wa kina wa soko la uwekezaji ili kuhakikisha mapato halisi ya uwekezaji yanaendelezwa. Kiwango cha mfumuko wa bei na mapato halisi ya Mfuko kwenye uwekezaji ni kama inavyoonyeshwa kwenye **Kielelezo cha 5**.

**Kielelezo cha 5:** Mwenendo wa Mapato ya Uwekezaji




#### 2.3.1.4 Gharama za Uendeshaji katika Uwiano wa Jumla wa Mapato

Mfuko una kikomo cha kutumia si zaidi ya asilimia 15 ya mapato yake yote kwa gharama za uendeshaji. Gharama za uendeshaji zinajumuisha mishahara ya wafanyakazi, gharama za ofisi, huduma, matumizi ya ofisi na uchapishaji, matengenezo ya programu, mafunzo ya wafanyakazi, safari za kazi, na gharama nyingine za kiutawala zinazowezesha utekelezaji wa shughuli katika Kurugenzi au Vitengo.

Katika kipindi cha mapitio, gharama za uendeshaji kwa uwiano wa jumla wa mapato zilikuwa chini ya kikomo cha udhibiti cha asilimia 15 (**Kielelezo cha 6**). Hata hivyo, kulikuwa na

mabadiliko ya uwiano hasa kutokana na ongezeko la gharama za uendeshaji kutokana na upanuzi wa uendeshaji wa Mfuko kama vile kufungua ofisi za kanda, kuajiri wafanyakazi wapya na kuendeleza na kuweka mfumo muhimu wa TEHAMA na miundombinu. Hata hivyo, katika mwaka 2021/22 kuna uwezekano wa Mfuko kutofikia ukomo uliowekwa kutokana na mabadiliko ya kiwango cha michango kutoka asilimia 1 hadi 0.6 kwa sekta binafsi jambo ambalo litaathiri ukusanyaji wa michango. Pamoja na mabadiliko yanayotarajiwa, Mfuko utaendelea kufuatilia kwa karibu vyanzo vyake vya mapato ili kuhakikisha matumizi yanabaki ndani ya ukomo uliowekwa.

**Kielelezo cha 6**: Mwenendo wa Uwiano wa Gharama za Uendeshaji




### 2.3.1.5 Kiwango cha Kubana Matumizi Katika Bajeti

Hatua hii inalenga kudhibiti gharama za uendeshaji bila kujali bajeti iliyoidhinishwa. Kiwango hiki kinapatikana kwa kulinganisha matumizi halisi dhidi ya bajeti iliyoidhinishwa kufikia mwisho wa kipindi cha kuripoti. Hii husaidia Mfuko kuongeza rasilimali bila kuathiri ubora wa utoaji huduma. Lengo la Mfuko lilikuwa kupata fedha zinazotokana na kubana bajeti ya angalau asilimia 2 kutoka katika bajeti iliyoidhinishwa kila mwaka. Katika kipindi chote cha mapitio, kiwango cha kubana matumizi katika bajeti ya Mfuko kilikuwa juu ya lengo (**Kielelezo cha 7**). Hata hivyo, katika mwaka 2018/19 na 2019/20 uwiano wa Bajeti ulikuwa juu yaani asilimia 16.16 na 17.45 mtawalia kutokana na ukweli kwamba Mfuko haukupokea idadi kubwa ya wafanyakazi waliotarajiwa kujiunga na Mfuko katika kipindi hicho. Mfuko utaendelea kutekeleza taratibu za kudhibiti gharama za uendeshaji bila kuathiri utendaji kazi.

**Kielelezo cha 7**: Kupunguza Matumizi katika Bajeti




## 2.4 Mtazamo wa Ndani wa Mfumo wa Utendaji Kazi

Mtazamo huu unaangalia taratibu na mazoea ya Mfuko. Lengo ni kuhakikisha uwazi, ufanisi na tija katika utoaji wa huduma.

### 2.4.1 Kuongeza wigo wa Wanachama

Lengo hili linakusudia kuhakikisha kuwa Mfuko unaimarisha usajili wa waajiri na kufuata sheria ili kuongeza idadi ya waajiri wanaochangia. Lengo hili hupimwa kwa ukadiriaji wa namna mwajiri anavyofuata sheria na asilimia ya waajiri waliosajiliwa.

#### 2.4.1.1 Upimaji wa Uzingatiaji wa Mwajiri

Kipimo hiki kinalenga kuhakikisha waajiri wote Tanzania Bara waliopo katika sekta rasmi wamesajiliwa na kuchangia kwenye Mfuko. Lengo ni kuhakikisha wafanyakazi wanalindwa katika kipindi chote cha ajira. Kiwango cha uzingatiaji hupatikana kwa kulinganisha idadi ya waajiri wanaochangia dhidi ya waajiri waliosajiliwa katika kipindi husika cha mapitio.

Lengo la Mfuko lilikuwa kufikia viwango vya uzingatiaji vya mwajiri vya angalau asilimia 80 kila mwaka. Mwaka 2017/18 waajiri waliochangia walikuwa 9,931 kati ya waajiri 14,836 waliosajiliwa, 2018/19 waajiri 16,676 kati ya waajiri 20,102 waliosajiliwa, 2019/20 waajiri 20,718 kati ya 22,502 waliosajiliwa na 2020/21 waajiri 22,602 kati ya waajiri 25,085 waliosajiliwa. Waajiri wanaochangia 2021/22 wanatarajiwa kuongezeka na kufikia 25,944 sawa na asilimia 90 ya waajiri wanaotarajiwa kusajiliwa.

Katika kipindi cha mapitio, viwango vya uzingatiaji wa waajiri vilikuwa vikiongezeka mwaka hadi mwaka isipokuwa mwaka 2020/21 (**Kielelezo cha 8**). Sababu kuu za kushuka kwa uzingatiaji kwa mwaka 2020/21 zilitokana na athari za UVIKO-19 ambayo ilisababisha kufungwa kwa baadhi ya biashara pamoja na waajiri kutowasilisha michango.

Hata hivyo, Mfuko utaendelea kushirikiana na Taasisi mbalimbali za Umma na wadau wengine muhimu ili kuhakikisha waajiri wote ambao hawajasajiliwa wanatambulika, kusajiliwa na kuchangia Mfuko pamoja na kuimarisha taratibu za ufuatiliaji wa waajiri ili kufikia kiwango cha asilimia 90 kinachotarajiwa ifikapo Juni 2022.

**Kielelezo cha 8:** Kiwango cha Uzingatiaji cha Waajiri




### 2.4.1.2 Asilimia ya Waajiri Waliosajiliwa

Hatua hii inalenga kuhakikisha waajiri wote Tanzania Bara katika sekta rasmi wamesajiliwa na Mfuko. Asilimia hiyo inapatikana kwa kulinganisha waajiri waliosajiliwa dhidi ya waajiri waliopo kwenye kanzidata ya Mfuko katika kipindi husika cha mapitio.

Lengo lilikuwa kusajili angalau asilimia 95 ya waajiri wote waliopo kwenye kanzidata ya Mfuko ifikapo mwishoni mwa Juni 2022. Usajili wa waajiri ulikuwa ukiongezeka katika kipindi chote cha mapitio na kufikia asilimia 90 ya waajiri wote walioko kwenye kanzidata ya mfuko kufikia mwishoni mwa Juni 2020/21 (**Kielelezo cha 9**). Mfuko ulifanikiwa kusajili waajiri 14,836 mwaka 2017/18, waajiri 20,102 mwaka 2018/19, waajiri 22,542 mwaka 2019/20, waajiri 25,085 mwaka 2020/21 na unatarajiwa kusajili waajiri 28,822 hadi Juni 2022. Hata hivyo, ufanisi uliopatikana ulichangiwa na jitihada za Mfuko ikiwa ni pamoja na kufanya uhamasishaji kwa waajiri kuhusu masuala ya Fidia kwa Wafanyakazi, uwekaji wa mifumo inayojiendesha ya utendaji kazi ya usajili na uchangiaji, kufanya kaguzi za mara kwa mara na kaguzi zinazoshirikisha taasisi zingine.
Mfuko utaendelea kushirikiana na Taasisi mbalimbali za Umma na wadau wengine muhimu ili kuhakikisha waajiri wote ambao hawajasajiliwa wanatambulika, wanasajiliwa na kuchangia kwenye Mfuko.

**Kielelezo cha 9**: Mwenendo wa Usajili wa Waajiri




## 2.4.2 Kuboresha Ufanisi wa Uendeshaji

Lengo hili linakusudia kuhakikisha kwamba walengwa wote wanaostahili fidia ya Mfuko wanalipwa stahiki zao kwa wakati bila ubaguzi. Lengo hili hupimwa kwa kutumia vigezo vifuatavyo: muda wa kushughulikia malipo ya madai, muda wa kushughulikia madai yaliyokataliwa kwa kukosa sifa, ubora wa taarifa na asilimia ya kiwango cha matumizi ya mifumo ya utendaji kazi ya kidijiti.

### 2.4.2.1 Muda wa Kushughulikia Malipo ya Madai

Muda wa kushughulikia malipo ya madai ni wastani wa idadi ya siku zinazotumika kushughulikia na kulipa madai. Muda wa kushughulikia madai huanza kutoka siku ambayo Mfuko unapokea taarifa ya madai na viambatisho vyote vinavyohitajika kabla ya tathmini ya kudai malipo. Lengo ni kuhakikisha madai yanalipwa kwa wakati ndani ya muda unaotakiwa. Hili huwezesha Mfuko kufuatilia madai yote yaliyopokelewa ambayo muda wa malipo unavuka matakwa ya kisheria ya siku 30.

Shabaha ya Mfuko ilikuwa kuchakata na kulipa asilimia 90 ya madai yaliyokamilika yakiwa na viambatisho vyote ndani ya siku 30. Katika kipindi cha mapitio, Mfuko ulilipa jumla ya madai 8,874 ifikapo Juni 2021. Kati ya madai yaliyolipwa, ni madai 2,405 tu sawa na asilimia 27.10 ndiyo yalilipwa ndani ya siku 30 huku madai 4,757 (53.61%) yakiwa ni madai mengi yaliyolipwa kati ya siku 31 hadi siku 90. Licha ya ukweli kwamba madai mengi yalilipwa kati ya siku 31 hadi 90 idadi ya madai yaliyolipwa ndani ya siku 1 hadi 30 yalikuwa yanaongezeka mwaka hadi mwaka (**Kielelezo cha 10**). Miongoni mwa sababu za muda wa kushughulikia madai kuwa zaidi ya siku 30 ni kutokuwepo kwa taarifa za kutosha za madai yaliyowasilishwa, baadhi ya watumishi kutofikia Unafuu wa Juu wa Matibabu wakati wa uhakiki, kuchelewa kwa baadhi ya watumishi kujitokeza kwa ajili ya tathmini ya athari pale inapohitajika na waajiri kuchelewa kutuma michango ya watumishi waliopata ajali ambao wamekamilisha nyaraka zinazohitajika.

Hata hivyo, ufanisi uliopatikana ulichangiwa na mipango ya Mfuko ikiwa ni pamoja na kuweka mfumo wa utendaji kazi unaojiendesha wenyewe, ikiwa ni pamoja na kutengeneza mfumo wa kutoa taarifa kwa mtandao, kutoa uhamasishaji na elimu kwa waajiri kwa wingi kuhusu masuala ya Fidia kwa Wafanyakazi na mapitio ya sheria na kanuni. Mfuko utaboresha Mfumo wa Utoaji Taarifa kwa Mtandao na kufanya usanifu upya wa mfumo wa utendaji kazi ili kuhakikisha asilimia 90 ya madai yanalipwa ndani ya siku 30 hadi Juni 2022.

**Kielelezo cha 10**: Muda wa Kutoa Majibu ya Madai na Jumla ya Madai Yaliyolipwa




### 2.4.2.2 Muda wa Kutoa Majibu ya Madai Yaliyokataliwa

Muda wa kutoa majibu ya madai yaliyokataliwa ambayo hayana sifa ni wastani wa idadi ya siku zinazohitajika kukagua na kukataa madai ambayo hayana sifa. Muda wa Kutoa Majibu huanza kuhesabiwa kuanzia siku ambayo Mfuko unapokea taarifa ya madai hadi siku ambayo madai yanakataliwa. Lengo ni kuhakikisha madai yasiyo na sifa yanakataliwa ndani ya muda unaotakiwa. Shabaha ya Mfuko ilikuwa ni kufanya mapitio ili kubaini madai yote ambayo hayana sifa na viambatisho na kuyakataa ndani ya siku 30.

Hadi kufikia Juni 2021 Mfuko ulikataa jumla ya madai 696. Kati ya madai yaliyokataliwa, madai 459 sawa na asilimia 65.88 yalikataliwa ndani ya siku 30, madai 198 (28.38%) yalikataliwa kati ya siku 31 hadi 90 na madai 40 yaliyosalia yalikataliwa baada ya siku zaidi 90 (**Kielelezo cha 11**). Mafanikio yaliyopatikana yalichangiwa na jitihada za Mfuko ikijumuisha mfumo wa utendaji kazi wa kidijiti wa madai na Mfumo wa Utoaji Taarifa kwa Mtandao. Mfuko utaboresha Mfumo wa utoaji taarifa kwa njia ya mtandao na kufanya uundaji upya wa mfumo wa utendaji kazi ili kuhakikisha asilimia 100 ya madai yenye viambatisho kamili yanapata majibu ndani ya siku 30 kufikia Juni 2022.

**Kielelezo cha 11**: Muda wa Kutoa Majibu ya Madai Yaliyokataliwa




#### 2.4.2.3 Kielezo cha Ubora wa Taarifa

Hatua hii inalenga kuhakikisha kwamba taarifa zote za Mfuko zina ubora wa hali ya juu ili kuwezesha kufanya maamuzi yenye tija. Lengo lilikuwa kufikia angalau asilimia 95 ya kielezo cha ubora wa taarifa ifikapo Juni 2022. Kwa miaka miwili ya kwanza ya Mpango wa 2017/18 na 2018/19, Mfuko ulikuwa bado haujaweka utaratibu wa kupata kielezo cha ubora wa taarifa hadi 2019/20. Kutokana na hali hiyo, mazoezi mawili (2) ya ubora wa taarifa yalifanyika (zoezi moja mwaka 2019/20 na lingine mwaka 2020/21) ili kubaini ubora wa taarifa zilizopo. Kiwango cha kielezo cha ubora wa data kwa vipindi vyote viwili vilikuwa asilimia 90.34 na 97.28, mtawalia. Mafanikio hayo yalichangiwa na jitihada za kufanya mazoezi ya mara kwa mara ya usafishaji wa taarifa. Ili kufikia kiwango cha ubora kwa asilimia 100 ifikapo Juni 2022, Mfuko utaimarisha ubora wa taarifa na kuendelea kufanya usafishaji wa taarifa mara kwa mara.

#### 2.4.2.4 Kiwango cha Kujiendesha kwa Mfumo wa Utendaji Kazi

Hatua hii inalenga kuhakikisha mifumo yote ya Mfuko ya utendaji kazi ambayo inaweza kufanywa ijiendeshe yenyewe inatengenezwa ili kuboresha utoaji wa huduma. Katika kipindi cha mapitio, lengo la Mfuko lilikuwa kufikia angalau kiwango cha asilimia 90.00 ya mifumo ya utendaji kazi inayojiendesha yenyewe kufikia Juni 2022.

Katika kipindi cha mpango, kiwango cha mifumo inayojiendesha ilikuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka na kufikia asilimia 85.70 Juni 2021. Mwaka 2017/18 kiwango cha mifumo inayojiendesha ilikuwa asilimia 58.00, 2018/19 ilikuwa asilimia 65.00, 2019/20 ilikuwa asilimia 84.00 na 2020/21 ilikuwa asilimia 85.70 (**Kielelezo cha 12**). Utendaji uliopatikana ulitokana na uboreshaji wa mfumo wa MAC, Tovuti ya Mfumo wa Kujihudumia Mtandaoni

(WCFePG Portal), Mfumo wa Kusimamia Mahusiano na Wateja, Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi vya Biashara, Mfumo wa Ufuatiliaji wa ICT, Mfumo wa Usafirishaji na Usimamizi wa Mali unaojumuisha moduli ya usimamizi wa mikataba ambayo imepunguza kwa kiasi kikubwa gharama na malalamiko ya waajiri hasa katika kuwasilisha marejesho ya mapato ya kila mwaka, mabadiliko ya maelezo ya waajiri na kuoanisha taarifa za wafanyakazi wengi.

Mfuko utaendelea kubainisha mifumo ya utendaji kazi ambayo haijatengenezwa ijiendeshe yenyewe ili kufikia kiwango cha mifumo kujiendesha yenyewe cha asilimia 90.00 ifikapo Juni 2022. Maelezo ya kiwango cha mifumo kujiendesha ni kama inavyoonekana kwenye kielelezo cha 12.

**Kielelezo cha 12:** Kiwango cha Mifumo ya Utendaji Kazi Inayojiendesha




**Jedwali la 1:** Maelezo ya Mifumo Inayojiendesha kufikia tarehe 30 Juni 2021

| **Maelezo** | **Hali ya Sasa** | |
|---|---|---|
| | **Namba** | **Asimilia** |
| Mfumo wa Utendaji Kazi (MUK) wa Jumla | 97 | 100% |
| MUK Isiyohitaji mfumo wa kujiendesha | 20 | 20.6% |
| MUK Inayohitaji mfumo wa kujiendesha | 77 | 79.4% |
| *MUK Inayojiendesha kwa ukamilifu* | *6* | *85.7%* |
| *MUK Inayojiendesha kwa sehemu* | *4* | *5.2%* |
| *MUK Ambayo haijiendeshi yenyewe* | *7* | *9.1%* |

### 2.4.2.5 Asilimia ya Utekelezaji wa Mpango wa Ununuzi wa Mwaka

Sheria ya Ununuzi inahitaji Mfuko kuandaa Mpango wa Ununuzi wa Mwaka (MUM) unaoonyesha maelezo ya bidhaa zote zinazoweza kununuliwa pamoja na zabuni husika kwa mwaka huo. Katika kuhakikisha ufanisi katika utoaji wa huduma, MUM inapaswa kutekelezwa kwa ufanisi. Kwa maana hiyo, lengo lilikuwa kutekeleza MUM kwa angalau asilimia 95 kila mwaka.

Kiwango cha utekelezaji kwa mwaka 2018/19 kilikuwa asilimia 66.10, kwa 2019/20 kilikuwa asilimia 76.14 na 87.18 kwa 2020/21 (**Kielelezo cha 13**). Kiwango cha utekelezaji kilikuwa kikiongezeka mwaka hadi mwaka licha ya kutofikia lengo lililowekwa la asilimia 95. Hii ilichangiwa na kucheleweshwa kwa uanzishwaji wa zabuni.

Hata hivyo, ufuatiliaji utaimarishwa kwa idara za watumiaji ili kuhakikisha sifa na vipimo kamili vinatolewa kwa wakati na zabuni zote zilizopangwa zinaanzishwa ili kufikia asilimia 95 ya utekelezaji wa MUM.

**Kielelezo cha 13:** Utekelezaji wa Mpango wa Ununuzi wa Mwaka




### 2.4.2.6 Imarisha Usimamizi wa Vihatarishi

Lengo hili linakusudia kuweka taratibu za usimamizi wa vihatarishi ndani ya shughuli za Mfuko ili kuimarisha mwendelezo wa biashara, kupunguza mazingira yanayoweza kusababisha vihatarishi na kuhakikisha utii wa sheria na sera. Lengo hupimwa kwa kielezo cha vihatarishi, asilimia ya kiwango cha uzingatiaji wa taasisi, kiwango cha Mamlaka ya Ununuzi (PPRA) na asilimia ya mapendekezo ya ukaguzi yaliyotatuliwa.

### 2.4.2.7 Kielezo cha Vihatarishi

Kielezo hiki hupima viashiria muhimu vya vihatarishi ambavyo vinazidi kiwango

kinachovumilika. Madhumuni ya hatua hii ni kuhakikisha kuwa Mfuko unafanya kazi ikiwa na kiwango himilivu cha vihatarishi katika kupitia malengo yake ya kimkakati. Lengo la Mfuko ni kuwa na chini ya asilimia 20 ya viashiria vya vihatarishi. Katika kipindi cha mapitio, hali inaonyesha kuwa kielezo cha vihatarishi kilikuwa ndani ya kiwango kinachokubalika isipokuwa mwaka 2018/19 ambapo kielezo cha vihatarishi kilikuwa asilimia 23.00 (**Kielelezo cha 14**). Utendaji uliopatikana ulichangiwa na utekelezaji na usimamizi wa vidhibiti vilivyowekwa kwa vihatarishi vilivyobainishwa. Hata hivyo, muda unaotumika kuchakata madai, ucheleweshaji wa kuidhinisha huduma ya matibabu na ucheleweshaji wa mrejesho wa mawasiliano kutoka kwa mwajiri ni miongoni mwa viashiria vikuu vilivyochangia kuongezeka kwa kielezo cha vihatarishi. Mfuko utaendelea kuandaa na kutumia njia za huduma za kielektroniki kama vile mfumo wa ankara za matibabu za watoa huduma za afya, Mfumo wa Utoaji Taarifa Mtandaoni na Mfumo wa usimamizi wa uhusiano na Wateja (CRM) ili kuhakikisha kuwa Kielezo cha vihatarishi kinabaki katika kiwango kinachokubalika.

**Kielelezo cha 14:** Mwenendo wa Hali ya Vihatarishi




### 2.4.3 Ukadiriaji wa Uzingatiaji wa Kitaasisi

Kielezo cha Utendaji cha Uzingatiaji wa Kitaasisi kinatokana na Ripoti ya Viashiria vya Uzingatiaji. Kielezo hupima uzingatiaji katika kategoria tano ambazo ni Kisheria, Udhibiti, Nyaraka za Ndani, Makubaliano na Kubadilishana Uzoefu. Nia ya hatua hii ni kuhakikisha kuwa Mfuko unazingatia sheria, mahitaji ya udhibiti na Sera za ndani katika utekelezaji wa shughuli zake. Lengo la Mfuko ni kufikia asilimia 100 ya kiwango cha Uzingatiaji wa Taasisi. Katika kipindi cha mapitio, kiwango cha uzingatiaji wa jumla wa Taasisi kilikuwa asilimia 96. Hii ina maana kwamba juhudi za Mfuko katika masuala ya uzingatiaji zimetoa matokeo yaliyokusudiwa ya kuhakikisha uzingatiaji wa asilimia 100 katika sera na sheria.

#### 2.4.3.1 Kiwango cha Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (MKUU)

Kiwango hiki hupima uzingatiaji wa Mfuko katika masuala ya ununuzi. Lengo ni kufikia angalau asilimia 95 ya alama za MKUU. Katika kipindi cha mapitio, Mfuko ulikaguliwa mara

moja kwenye masuala ya ununuzi. Ukaguzi ulifanyika katika kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2019. Kwa mujibu wa matokeo ya ukaguzi, Mfuko ulipata asilimia 88.20 kama kiwango cha MKUU. Sababu kuu za kiwango hiki cha ufanisi ni watumiaji kuchelewa kuanzisha zabuni hali iliyosababisha kuchelewa kwa utekelezaji wa MUM.

#### 2.4.3.2 Asilimia ya Mapendekezo ya Ukaguzi Yaliyotekelezwa

Mapendekezo ya Ukaguzi ni maagizo yanayotolewa na taasisi ya ukaguzi kwa taasisi iliyokaguliwa kwa ajili ya utekelezaji katika muda maalumu. Hatua hiyo inakusudia kufuatilia kiwango cha utekelezaji wa mapendekezo yote yaliyopokelewa. Lengo ni angalau asilimia 80 ya mapendekezo ya ukaguzi yatekelezwe kila mwaka.

Katika kipindi cha mapitio, kiwango cha Mfuko katika utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yalikuwa juu ya lengo la mapendekezo ya mkaguzi wa ndani na nje. Mapendekezo ya ukaguzi wa ndani yalitekelezwa kwa asilimia 85.45 na mapendekezo ya ukaguzi wa nje yalitekelezwa kwa asilimia 84.06. Mapendekezo ambayo bado hayajatekelezwa yanayotokana na ukaguzi wa nje ni pamoja na michango ambayo haijalipwa, michango isiyosajiliwa, kiasi kikubwa cha malipo yanayosubiri kufanyika na marejesho ya michango kwa waajiri. Mapendekezo ya ukaguzi wa ndani ambayo hayajatekelezwa ni pamoja na uhakiki wa wastaafu wa nje ya nchi, utayarishaji wa mwongozo wa usimamizi wa mali na mkataba wa wafanyakazi waliopo katika muda wa mafunzo. Katika kuhakikisha mapendekezo yote yanatekelezwa kwa wakati, Mfuko utahakikisha usimamizi wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi unaimarishwa.

### 2.4.4 Kukuza Afya na Usalama Mahali pa Kazi

Lengo hili linakusudia kuhakikisha kuwa waajiri wanajitahidi kujenga mazingira salama ya kazi na hivyo kupunguza ajali na vifo kwa watumishi na kujenga utamaduni wa kuwekea kinga dhidi ya ajali na magonjwa yanayoweza kuepukika mahali pa kazi. Lengo hili linapimwa kwa kuangalia asimilia ya kupungua kwa ajali au magonjwa mahali pa kazi.

#### 2.4.4.1 Asilimia ya kupungua kwa Ajali na Magonjwa Mahali Pakazi

Kipimo hiki kinalenga kupunguza ajali na magonjwa mahali pa kazi kupitia mipango inayofanywa na Mfuko na waajiri. Kipimo hiki kinapimwa kwa kuzingatia taarifa zinazotokana na tafiti za matukio ya ajali na magonjwa mahali pa kazi. Lengo ni kupunguza ajali na magonjwa mahali pa kazi kwa angalau asilimia 10 kwa waajiri waliopatiwa mafunzo.

Katika kipindi cha mapitio, Mfuko umefanya tafiti kuhusu ajali na magonjwa mahali pa kazi kwa waajiri walio katika hatari kubwa kwa miaka mitatu yaani mwaka 2018/19, 2019/20 na 2020/21. Kwa mwaka 2018/19 na 2019/20 matukio ya ajali na magonjwa mahali pa kazi hayakupungua tofauti na mwaka 2020/2021 ambapo matukio hayo yalipungua kwa asilimia 6.97. Kupungua kwa matukio katika mwaka 2020/2021 kulitokana na juhudi zilizofanywa na Mfuko ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi na waajiri kuhusu afya na usalama mahali pa kazi na masuala ya fidia kwa wafanyakazi na kufanya ukaguzi wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi kwa waajiri wenye mazingira ya kazi hatari zaidi.

**Kielelezo cha 15:** Asilimia ya Kupungua kwa Matukio ya Ajali Mahali pa Kazi




### 2.4.5 Kuboresha Usimamizi wa Uhusiano na Washirika

Lengo hili linakusudia kuhakikisha kuwa Mfuko unaendelea kuboresha ushirikiano na washirika wake kwa kubadilishana taarifa, uzoefu, utendaji bora na msaada wa kiufundi. Lengo hili hupimwa kwa asilimia ya utekelezaji wa Hati za Mikataba ya washirika.

#### 2.4.5.1 Asilimia ya Makubaliano ya Washirika Yaliyotekelezwa

Mkataba wa Makubaliano husaidia Mfuko kuboresha huduma zake kupitia ubadilishanaji taarifa na ujuzi baina ya washirika. Kipimo hiki kinakusudia kufuatilia kiwango cha ushirikiano uliokubaliwa kati ya Mfuko na Washirika.

Hadi kufikia kipindi cha mapitio, utekelezaji wa makubaliano na washirika mbalimbali ulikuwa kwa asilimia 100. Mafanikio hayo yalichangiwa na ushirikiano mzuri kati ya Mfuko na washirika husika. Miongoni mwa washirika wakuu ambao Mfuko ulikuwa umetia saini Makubaliano nao ni pamoja na; DGUV-German (mwaka 2018/219), WCFCB-Zambia (2019/20), OSHA, NSSF, TRA, NHIF, GPSA, TCDC, NIDA, Wizara ya Maliasili na Utalii na Jeshi la Polisi (2020/21). Aidha, Mfuko upo katika taratibu za kusaini makubaliano na RITA. Mfuko utaendelea kushirikiana na Wadau wote wa Kimkakati katika utoaji wa huduma bora.

## 2.5 Mtazamo wa Kujifunza na Ukuaji

Mtazamo wa Kujifunza na Ukuaji unajikita katika kuwawezesha wafanyakazi kupata maarifa, ujuzi na umahiri unaohitajika ili kutimiza malengo ya Mfuko. Juhudi katika mtazamo huu zinajikita katika utoaji wa mafunzo mbalimbali ambayo yana umuhimu katika kutekeleza majukumu ya Mfuko kwa lengo la kuwawezesha wafanyakazi kuziba pengo la maarifa

litakalobainika.

### 2.5.1 Kuimarisha Utawala

Lengo hili linakusudia kuboresha jinsi Mfuko unavyodhibitiwa na kuelekezwa kwa kuweka mikataba, mifumo, sera na mikakati ambayo itaimarisha udhibiti wa ndani wa Mfuko. Lengo hili linapimwa kwa matokeo ya ripoti ya ukaguzi na kiwango cha utekelezaji wa Mpango kwa Mwaka.

#### 2.5.1.1 Matokeo ya Ripoti ya Ukaguzi

Kipimo hiki kinaangalia matokeo yanayotolewa na mkaguzi wa nje (Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali – CAG) kwa taasisi iliyokaguliwa baada ya zoezi la ukaguzi kukamilika. Zoezi la ukaguzi hufanywa kila mwaka. Lengo la Mfuko lilikuwa ni kupata Hati Safi ya Ukaguzi kila mwaka.

Katika kipindi cha mapitio, Mfuko umefanyiwa kaguzi nne (4) na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kati miaka 2015/16 - 2019/20. Katika kaguzi zote, Mfuko umepata hati safi za ukaguzi ikiwa ni asilimia 100 ya lengo. Mafanikio yaliyopatikana yanatokana na usimamizi madhubuti wa Mfuko.

#### 2.5.1.2 Kiwango cha Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka

Mpango wa Mwaka unajumuisha malengo na shughuli zote ambazo zimeidhinishwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha husika. Lengo la Mfuko lilikuwa kutekeleza Mpango wa Mwaka kwa asilimia 80 ifikapo 2022. Katika kipindi chote cha utekelezaji, utekelezaji wa Mpango wa Mwaka ulikuwa juu ya lengo (**Kielelezo cha 16**). Mafanikio hayo yalichangiwa na jitihada za wafanyakazi katika kuhakikisha mipango inatekelezwa ipasavyo.

**Kielelezo cha 16:** Mwenendo wa Mpango wa Utekelezaji wa Mwaka



### 2.5.2 Kuboresha Ujuzi na Maarifa kwa Wafanyakazi

Lengo hili linakusudia kuongeza tija ya Mfuko kwa kuwapa uwezo wafanyakazi kupitia fursa za kujifunza na kujiendeleza na kwa kuunganisha programu za mafunzo na mpango wa kurithishana madaraka, kuwajengea uelewa mpana, kuweka programu za kuwakuza wafanyakazi wa ngazi za chini kitaalamu na kuwawezesha kufikia malengo mkakati ya Mfuko. Lengo hili linapimwa kwa kiwango cha utendaji wa wafanyakazi.

#### 2.5.2.1 Kiwango cha Utendaji Kazi wa Wafanyakazi

Utendaji wa wafanyakazi ni uwezo wa mfanyakazi kutoa matokeo yaliyokusudiwa ndani ya muda na kwa kutumia rasilimali zilizotolewa. Lengo la kipimo hiki ni kuhakikisha wastani wa utendaji kazi wa wafanyakazi ni wa kiwango cha juu ili kufikia malengo ya Mfuko. Lengo ni kufikia angalau kiwango cha alama 2 za utendaji kazi wa wafanyakazi kila mwaka. Katika kipindi cha mapitio, kiwango cha jumla cha utendaji wa wafanyakazi kilikuwa kama kinavyoonekana katika **Kielelezo Na. 17**. Miongoni mwa mambo muhimu yaliyochangia mafanikio hayo ni pamoja na mafunzo kwa watumishi kwa wakati, mazingira mazuri ya kazi pamoja na kuwepo kwa utawala bora.

**Kielelezo cha 17:** Utendaji wa Wafanyakazi




***Angalizo**: Ukadiriaji wa utendaji kazi wa wafanyakazi umefafanuliwa kama ifuatavyo: 1 inamaanisha utendaji kazi bora, 2 inamaanisha utendaji kazi uliozidi wastani, 3 inamaanisha utendaji kazi wa wastani, 4 inamaanisha utendaji kazi duni na 5 unamaanisha utendaji kazi duni sana.*

## 2.5.3 Kuboresha Mazingira na Utamaduni wa Kazi

Lengo hili linakusudia kuweka mazingira ya kazi ambayo yanakuza utamaduni wa utendaji, uvumbuzi, ubunifu na utoaji vitendea kazi pamoja na teknolojia sahihi ili kuwezesha wafanyakazi kutekeleza malengo ya shirika ipasavyo. Lengo hili hupimwa kwa kuangalia kiwango cha kuridhika kwa wafanyakazi, asilimia ya mawazo bunifu yaliyotekelezwa na kiwango cha ukomavu wa utamaduni wa utendaji kazi.

### 2.5.3.1 Kiwango cha Kuridhika kwa Wafanyakazi

Kipimo hiki kinalenga kuhakikisha kuwa wafanyakazi wanaridhishwa na mazingira ya kazi ili kuongeza tija. Kipimo hiki ni mrejesho kutoka kwa wafanyakazi kuhusu hali ya mazingira ya kazi. Kiwango hiki hupatikana kwa tafiti zinazofanywa kila mwaka ili kupima kiwango cha kuridhika kwa wafanyakazi. Lengo la Mfuko lilikuwa kufikia kiwango cha kuridhika kwa wafanyakazi cha asilimia 80 kila mwaka.

Katika kipindi cha mapitio, alama za kuridhika kwa wafanyakazi zilikuwa zikibadilika kama inavyoonyeshwa kwenye **Kielelezo cha 18**. Kuongezeka kwa hali ya kuridhika kwa wafanyakazi kulitokana na jitihada za Mfuko za kuhakikisha watumishi wanapatiwa vitendea kazi na huduma zote muhimu pamoja na mafunzo mbalimbali yaliyotolewa kwa wafanyakazi na warsha za kujenga ujuzi wa maisha na kazi. Mfuko utaendelea kutekeleza mipango mbalimbali kama vile utekelezaji wa programu za ustawi wa jamii na mipango ya maendeleo ya rasilimali watu ili kufikia kiwango cha kuridhisha cha asilimia 90 ifikapo Juni 2022.

**Kielelezo cha 18:** Kiwango cha Kuridhika kwa Wafanyakazi



## 2.6 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MSINGI

<table>
<tr><th rowspan="2">Malmlaka ya Mfuko</th><th colspan="2">Mapitio</th></tr>
<tr><th>Mafanikio</th><th>Vikwazo</th></tr>
<tr>
<td rowspan="3">(a) Utoaji wa fidia toshelevu na kwa usawa kwa wafanyakazi.<br><br>Maelezo<br><br>Madhumuni ya jukumu hili ni kuhakikisha kuwa Mfuko unatoa mafao ambayo yanakidhi mahitaji ya wafanyakazi waliojeruhiwa na ambayo yanaendana na viwango vya kimataifa.</td>
<td>Mafanikio ya Jumla<br><br>(i) Tathmini ya jumla ya utoshelevu inapimwa kwa kuangalia uwiano kati ya kipato cha mfanyakazi na fidia ambapo kiwango cha chini kwa mujibu wa ILO ni asilimia 60. Kiwango cha chini cha sasa cha uwiano kati ya kipato cha mfanyakazi na fidia kinacholipwa na Mfuko ni asilimia<br><br>Mafanikio Mahususi<br><br>(i) Katika kipindi cha mapitio, Mfuko ulilipa Shilingi bilioni 30.62 kwa watumishi waliopata ulemavu kutokana na kazi na kwa wategemezi wa wafanyakazi waliofariki kutokana na ajali au magonjwa yatokanayo na kazi.<br><br>(ii) Idadi ya mafao yanayotolewa yanalingana na viwango vya kimataifa<br><br>(iii) Kuzingatiwa kwa kanuni ya usawa kumepelekea kutokuwepo kwa ubaguzi wa huduma kati ya walengwa.</td>
<td>(i) Waajiri kutozingatia kima cha chini cha mshahara wa kisekta kilichopendekezwa.<br><br>(ii) Uelewa mdogo kuhusu mafao unaosababisha matarajio yasiyo ya kweli miongoni mwa walengwa<br><br>(iii) Wigo mdogo wa huduma za utengemao zinazotolewa.</td>
</tr>
<tr><td colspan="2">Mapendekezo ya Namna ya Kusonga Mbele</td></tr>
<tr><td colspan="2">(i) Kupendekeza waajiri kuzingatia kima cha chini cha mshahara ya kisekta<br>(ii) Kuongeza ufahamu juu ya mafao ya Mfuko<br>(iii) Kufanya ongezeko la pensheni kulingana na mfumuko wa bei kwa vipindi.<br>(iv) kuboresha fao la utengemao</td></tr>
</table>

<table>
<tr><th rowspan="2">Malmlaka ya Mfuko</th><th colspan="2">Mapitio</th></tr>
<tr><th>Mafanikio</th><th>Vikwazo</th></tr>
<tr><td rowspan="3">(b) Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2003 kuhusiana na majeraha, magonjwa na vifo vinavyotokana na kazi.<br><br>Maelezo<br><br>Lengo kuu la Sera ni kuunda mfumo wa kisheria wa kupanua wigo wa hifadhi ya jamii kwa wafanyakazi wote katika sekta rasmi na kubuni njia za kupanua wigo wa sekta isiyo rasmi kama vile kilimo, madini, uvuvi na biashara ndogo ndogo.</td><td>Mafanikio ya Jumla<br><br>Kuanzishwa kwa Mfuko wa Fidia unaojitegemea (WCF) unaotoa mafao ya ajali mahali pa kazi kwa wafanyakazi yanayokidhi viwango vilivyowekwa.<br><br>Mafanikio mahususi<br><br>(i) Kulipa Mafao kwa wanufaika wa ndani na nje ya nchi<br><br>(ii) Kuongezwa kwa wigo wa huduma</td><td>(i) Kutokuwepo kwa mfumo wa kisheria unaokubalika kimataifa wa kuwezesha uhamishaji wa mafao ya hifadhi ya jamii kwa wafanyakazi.<br><br>(ii) Changamoto ya uhakiki wa wanufaika nje ya mipaka ya nchi.<br><br>(iii) Kutofikiwa kwa wafanyakazi katika sekta isiyo rasmi<br><br>(iv) Kasi ndogo ya ongezeko la ajira rasmi<br><br>(v) Viwango vya chini vya mapato miongoni mwa wafanyakazi<br><br>(vi) Waajiri kutoa taarifa ya vipato vya wafanya-kazi chini ya kiwango halisi.</td></tr>
<tr><td colspan="2">Mapendekezo ya Namna ya Kusonga Mbele</td></tr>
<tr><td colspan="2">(i) Kuanzisha kwa mfumo wa kisheria unaokubalika kutoka taifa moja kwenda jingine utakaowezesha uhamishaji wa mafao ya hifadhi ya jamii kimataifa.<br><br>(ii) Kusogeza huduma za Mfuko kwa kufungua matawi<br><br>(iii) Kutathmini uwezekano wa kupanua wigo kwa sekta isiyo rasmi<br><br>(iv) Kufikiria jinsi ya kuongeza wigo wa Mfuko kwa watu waliojiajiri<br><br>(v) Kushinikiza uwasilishaji wa michango.</td></tr>
</table>

<table>
<tr><th rowspan="2">Malmlaka ya Mfuko</th><th colspan="2">Mapitio</th></tr>
<tr><th>Mafanikio</th><th>Vikwazo</th></tr>
<tr>
<td rowspan="3">(c) Kuweka mfumo wa ulipaji mafao unaozingatia ufanisi,<br>haraka na kwa kuzingatia utu.<br><br>Maelezo<br><br>Kuwezesha mfumo madhubuti wa ulipaji mafao wenye ufanisi.</td>
<td>Mafanikio ya jumla.<br><br>Mfumo wa malipo ya mafao upo na unatekelezwa.<br><br>Mafanikio mahususi<br><br>(i) Mfumo wa kuwasilisha madai kwa njia ya mtandao umeanzishwa na kutekelezwa.<br><br>(ii) ii. Mtandao wa watoa huduma umeongezwa.</td>
<td>(i) Muda wa kushughulikia madai kuwa mrefu<br><br>(ii) Uelewa mdogo kuhusu mafao unaosababisha matarajio yasiyo ya kweli kwa walengwa<br><br>(iii) Idadi ndogo ya madaktari waliobobea kwenye tathmini ya ulemavu wa mwili<br><br>(iv) Kukosekana kwa mfumo wa utambulisho wa wadai kwa Watoa Huduma za Afya<br><br>(v) Vitendo vya udanganyifu katika malipo ya madai</td>
</tr>
<tr><td colspan="2">Mapendekezo ya Namna ya Kusonga Mbele</td></tr>
<tr><td colspan="2">(i) Kupitia na kuboresha mtiririko wa malipo ya mafao<br><br>(ii) Kuhakikisha mifumo ya kidijiti inatumika katika uchakataji wa madai<br><br>(iii) Kuongeza uelewa kuhusu Mafao yanayotolewa na Mfuko<br><br>(iv) Kutoa mafunzo ya kujenga uwezo kwa madaktari katika maeneo ya ajali au magonjwa mahali pa kazi<br><br>(v) Kufanikisha mawasiliano ya mifumo ya Mfuko na watoa huduma kupitia teknolojia<br><br>(vi) Kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ulaghai</td></tr>
</table>

<table>
<tr><th rowspan="2">Malmlaka ya Mfuko</th><th colspan="2">Mapitio</th></tr>
<tr><th>Mafanikio</th><th>Vikwazo</th></tr>
<tr><td rowspan="3">(d) Kuweka mfumo wa usimamizi na udhibiti wa ukusanyaji wa michango na ulipaji<br><br>Maelezo<br><br>Kuwezesha ukusanyaji wa michango na ulipaji wa madeni.</td><td>Mafanikio ya Jumla<br><br>Tangu kuanzishwa kwake Mfuko umefanikiwa kukusanya Shilingi bilioni 462.07 kutoka sekta binafsi na za umma.<br><br>Mafanikio Mahususi<br><br>(i) Ushirikiano na wadau wengine kama vile TRA, NSSF, BRELA katika kuboresha kanzidata ya waajiri.<br><br>(ii) Kuboresha na kuendeleza utekelezaji wa programu za ukaguzi wa pamoja na wadau kama vile PMO-LYED, OSHA na NSSF.</td><td>(i) Uwepo wa waajiri wasiotekeleza wajibu wa kisheria<br><br>(ii) Idadi ndogo ya Watumishi wa kufuatilia michango<br><br>(iii) Athari za UVIKO-19 kwenye ukusanyaji wa michango</td></tr>
<tr><td colspan="2">Mapendekezo ya Namna ya Kusonga Mbele</td></tr>
<tr><td colspan="2">(i) Kuimarisha ushirikiano wa kimkakati ili kuongeza ukusanyaji wa michango.<br><br>(ii) Kuwezesha uunganishaji wa mifumo ili kuboresha ukusanyaji na ulipaji wa fidia</td></tr>
</table>

| Malmlaka ya Mfuko | Mapitio | |
|---|---|---|
| | **Mafanikio** | **Vikwazo** |
| (e) Kuhamasisha uzuiaji wa ajali na magonjwa yatokanayo na kazi.<br><br>**Maelezo**<br><br>Madhumuni ya lengo hili ni kuhakikisha uzingatiaji wa kutosha katika masuala ya usalama na afya ili kupunguza matukio ya ajali, magonjwa au vifo vinavyotokana na kazi. | **Mafanikio ya Jumla**<br><br>Semina za uhamasishaji kuhusu usalama na afya mahali pa kazi zilifanyika, ambapo jumla ya waajiri 1,493 walio na mazingira ya kazi hatarishi na wafanyakazi 11, 903 kutoka kwa waajiri hao wamefikiwa katika kipindi cha ukaguzi.<br><br>**Mafanikio Mahususi**<br><br>(i) Hatua mbalimbali zinazohusu afya na usalama mahali pa kazi zilichukuliwa zikiwahusisha waajiri waliopo katika kundi lenye vihatarishi vikubwa.<br><br>(ii) Kuboreshwa kwa ushirikiano kati ya mfuko na wadau wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi kupitia Mikataba ya Makubaliano (MoU) kuhusu shughuli za pamoja za kuboresha usalama na afya mahali pa kazi.<br><br>(iii) Usimamizi wa data za usalama na afya kazini. | (i) Idadi ndogo ya watumishi wa kutoa elimu kuhusu kuzuia ajali na magonjwa yanayotokana na kazi<br><br>(ii) Utekelezaji duni wa sheria za usalama na afya miongoni mwa wahusika.<br><br>(iii) Kutokuwa tayari kuweza katika usalama na afya kazini miongoni mwa waajiri. Uelewa mdogo juu ya masuala ya usalama na afya. |
| | **Mapendekezo ya Namna ya Kusonga Mbele** | |
| | (i) Kuimarisha ushirikiano na OSHA na wadau wengine katika masuala ya kuzuia ajali na magonjwa yanayotokana na kazi<br>(ii) Kufikiria kuanzisha utaratibu wa motisha kwa waajiri<br>(iii) Kuimarisha utoaji wa elimu ya usalama na afya mahali pa kazi (OSH) na usambazaji wa taarifa kuhusu OSH.<br>(iv) Kuanza kutoa elimu kuhusu Mkakati wa Kuzuia Ajali na Magonjwa sehemu za kazi (Prevention Strategy) wa Mfuko<br>(v) Utekelezaji wa kampeni ya dira ya dunia ya kupunguza vifo mahali pa kazi (Vision Zero)<br>(vi) Kuimarisha matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma za kuzuia ajali na magonjwa yatokanayo na kazi<br>(vii) Boresha Usimamizi wa Data za OSH (Ripoti ya Mwaka ya Data za OSH) | |

<table>
<tr><th rowspan="2">Malmlaka ya Mfuko</th><th colspan="2">Mapitio</th></tr>
<tr><th>Mafanikio</th><th>Vikwazo</th></tr>
<tr><td rowspan="3">(f) Utoaji wa huduma za utengemao<br><br>Maelezo<br><br>Kuimarisha hali ya kiafya ya wafanya-kazi waliojeruhiwa kwa kumwezesha kupona haraka na kurudi kazini</td><td>Mafanikio ya Jumla<br><br>Huduma za utengemao wa kitabibu zinatolewa kupitia watoa huduma walio na mikataba ya kutoa huduma hizo.<br><br>Mafanikio Mahususi<br><br>(i) Mkakati wa utengemao umeandaliwa<br><br>(ii) Ushirikiano wa kimkakati umeanzishwa ili kuimarisha huduma za utengemao<br><br>(iii) Mafunzo yametolewa kwa madaktari kuhusu huduma za utengemao.</td><td>(i) Huduma za utengemao kutojitosheleza<br><br>(ii) Idadi ndogo ya vituo vyenye uwezo wa kutoa huduma za utengemao zilizokamilika<br><br>(iii) Kiwango kidogo cha uelewa wa madaktari kuhusu ujuzi wa matibabu ya utengemao</td></tr>
<tr><td colspan="2">Mapendekezo ya Namna ya Kusonga Mbele</td></tr>
<tr><td colspan="2">(i) Kutekeleza Mkakati wa Utengemao<br><br>(ii) Kuongeza ubia wa kimkakati ili kuimarisha kazi ya Utengemao<br><br>(iii) Kuwajengea uwezo madaktari kuhusiana na matibabu ya utengamano.</td></tr>
</table>

| Malmlaka ya Mfuko | Mapitio | |
|---|---|---|
| | **Mafanikio** | **Vikwazo** |
| (g) Kutimiza wajibu wa kimataifa kuhusiana na fidia kwa wafanyakazi<br><br>**Maelezo**<br><br>Lengo kuu ni kuhakikisha kuwa shughuli za Mfuko zinaendana na viwango vya kimataifa na utaratibu bora. | **Mafanikio ya Jumla**<br><br>Mafao yanayotolewa na Mfuko yanakidhi matakwa ya mkataba wa Shirika la Kazi Duniani Na.121 wa 1964.<br><br>**Mafanikio Mahususi**<br><br>(i) Kulingana na tathmini ya uhai na uendelevu wa Mfuko, Hali ya kifedha ya Mfuko ni mzuri kifedha na ni endelevu.<br><br>(ii) Mfuko umeweza kulipa fidia kwa viwango vikubwa kuliko viwango vilivyoainishwa katika Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi ya mwaka 1949.<br><br>(iii) Mfuko umeweza kukidhi matakwa ya Sera ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2003. | (i) Kutoridhiwa kwa mikataba ya Shirika la Kazi Na. 102 na 121.<br><br>(ii) Ushirikiano mdogo kati ya Mfuko na mashirika ya kimataifa |
| | **Mapendekezo ya Namna ya Kusonga Mbele** | |
| | (i) Kuidhinisha mikataba husika<br><br>(ii) Kuimarisha ushirikiano na taasisi zinazofanana (za kimataifa/kikanda) kwa ajili ya uwekaji wa alama ya misingi<br><br>(iii) Kuendesha programu za kuwajengea uwezo wadau | |

## 2.7 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO 2016-2021

Mbali na Mpango Mkakati, Mfuko pia ulipitia mchango wake katika utekelezaji wa malengo husika ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP II-2016-2021). Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano awamu ya pili (2016-2021) ulikuwa na malengo tisa (9). Kati ya hayo, Mfuko ulikuwa na michango katika malengo matatu (3) yafuatayo.

### 2.7.1 Kujenga Msingi wa Kuigeuza Tanzania kuwa Taifa la Uchumi wa Kati wa Kiviwanda ifikapo 2025

Mfuko ulikuwa na michango miwili mikuu katika lengo hili mahususi. Kwanza, Mfuko ulihakikisha kuwa wafanyakazi waliopata majeraha katika utekelezaji wa majukumu yao ya kikazi wanalipwa fidia stahiki kwa mujibu wa Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi. Katika kipindi cha mapitio, Mfuko ulipokea jumla ya madai 9,597. Aidha, Mfuko ulitumia Shilingi bilioni 30.62 kulipia fidia kwa wanufaika wanaostahili. Mwenendo wa madai katika kipindi hicho ni kama inavyoonekana hapa chini.

**Jedwali la 2**: Mwenendo wa Madai

| Aina ya Madai | 2016 /17 | 2017 /18 | 2018 /19 | 2019/20 | 2020/21 | Total |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Ajali mahali pa Kazi | 721 | 1,355 | 1,853 | 2,140 | 2,406 | 8,475 |
| Magonjwa yatokanayo na kazi | 20 | 139 | 119 | 142 | 198 | 618 |
| Vifo vitokanavyo na kazi | 36 | 67 | 98 | 160 | 143 | 504 |
| **Jumla ya Madai** | **777** | **1,561** | **2,070** | **2,442** | **2,747** | **9,597** |

Pili, Mfuko upo katika hatua za awali za kufanya tathmini ya uwekezaji katika miradi mbalimbali ya viwanda. Hizi ni pamoja na kiwanda cha Chai cha Mponde kilichopo Tanga, Morogoro Canvas cha Morogoro na kiwanda cha bidhaa za matibabu cha Simiyu mkoani Simiyu. Hadi sasa kiwanda cha chai cha Mponde kipo katika hatua za awali za utekelezaji huku miradi iliyobaki ikifanyiwa tathmini ya uwekezaji.

### 2.7.2 Kuboresha ubora wa maisha na ustawi wa binadamu

Mfuko una wajibu wa kuhakikisha kwamba wafanyakazi wanaopata majeraha yatokanayo na kazi wanapata fidia stahiki, yenye kuzingatia usawa na kwa wakati. Msingi wa malipo ya fidia ni kuhakikisha kwamba kuna ulinzi wa kutosha wa nguvukazi kiasi kwamba wafanyakazi na/au wategemezi wa wafanyakazi wanaopata ajali zinazotokana na kazi, magonjwa au vifo wanaendelea kuishi maisha ya staha pamoja na kujali utu wao baada ya kuumia kazini au kwa wategemezi baada ya mfanyakazi kufariki. Katika kipindi cha mapitio, Mfuko umeendelea kulipa fidia kwa watumishi waliojeruhiwa na wategemezi kwa njia endelevu. Walionufaika

na fidia wamekuwa wakiendelea kujishughulisha na shughuli mbalimbali za kiuchumi hivyo kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa Taifa. Mwenendo wa fidia zinazolipwa katika kipindi cha mapitio ni kama ifuatavyo.

**Kielelezo cha 19:** Mwenendo wa Malipo ya Fidia




Aidha, kama njia ya kutimiza Wajibu wake wa Kijamii, Mfuko ulifanya shughuli mbalimbali zikiwemo kusaidia sekta ya afya, sekta ya elimu na vyuo vya ufundi stadi vinavyohudumia watu wenye ulemavu.

### 2.7.3 Kuhakikisha Mikataba ya Kimataifa na Kikanda Inatekelezwa kwa manufaa ya nchi

Mfuko unashiriki katika kuhakikisha mikataba ya kimataifa na kikanda (k.m. Ajenda ya Afrika 2063 na SDGs) inakuwa sehemu ya mipango ya maendeleo ya kitaifa na mifumo ya utekelezaji kwa manufaa ya nchi. Moja ya malengo ya Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi kwa mujibu wa Kifungu cha 3 (e) cha Sheria hiyo, ni kutekeleza majukumu ya kimataifa kuhusu malipo ya fidia kwa wafanyakazi. Kwa hiyo, shughuli za Mfuko huo zinafanywa kwa kuzingatia mikataba mbalimbali ya kimataifa ambayo nchi imeridhia. Mikataba hii ni pamoja na Mkataba Na. 102 na ILO wa 1952 kuhusu viwango vya chini vya Hifadhi ya Jamii, Mkataba wa ILO Na. 121 wa 1964 kuhusu majeraha ya ajira na Pendekezo la 202 la 2012 la ILO kuhusu viwango vya Hifadhi ya Jamii.

Mbali na nyenzo zilizotajwa, utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Mfuko unachangia kufikiwa kwa matarajio ya Umoja wa Afrika kupitia Ajenda 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu. Kuhusu Ajenda ya Afrika 2063, Mfuko unafuata mahitaji ya lengo namba 1 (Maisha yenye ubora wa hali ya juu, ubora wa maisha na ustawi wa wananchi wote), lengo la 3 (Wananchi wenye afya njema na lishe bora), lengo la 4 (Uchumi uliopitia mabadiliko), lengo

la 9 (Taasisi za fedha za Mabara zimeanzishwa na zinafanya kazi) na lengo la 12 (Taasisi zenye uwezo na uongozi wa mabadiliko uliopo). Malengo Husika ya Maendeleo Endelevu ni pamoja na lengo la 1 (Kukomesha umasikini katika aina zake zote kila mahali duniani) na lengo la 8 (Kukuza Ukuaji wa Uchumi endelevu, shirikishi, ajira kamili na yenye tija na kazi zenye kujali utu na heshima kwa wote).

## 2.8 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA CHAMA TAWALA 2015-2020 NA DIRA YA MAENDELEO YA TAIFA 2025

Mfuko pia umetekeleza matakwa ya Ilani ya Chama Tawala na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 kama ifuatavyo.

### 2.8.1 Maisha Bora na Mapambano dhidi ya Umaskini

Mfuko kupitia malipo ya mara kwa mara ya mafao kwa walengwa wanaostahili umechangia kufikia Kifungu cha 16 cha Ilani kuhusu mapambano dhidi ya umaskini na Lengo la 1 la Dira ya Maendeleo ya 2025 kuhusu maisha bora kwa kuhakikisha kuwa waathirika hawarudi katika umaskini. Katika kipindi cha mapitio, Mfuko umefanikiwa kushughulikia na kulipa mafao ya jumla ya Shilingi bilioni 30.62.

### 2.8.2 Utoaji wa Huduma Bora

Mfuko umeboresha njia zake za utoaji huduma kwa kutumia TEHAMA kulingana na kifungu cha 174(i)(i) cha Ilani. Katika kipindi cha mapitio, Mfuko ulifanikiwa kutumia TEHAMA katika mifumo yake ya utendaji kazi kwa asilimia 85.40.

### 2.8.3 Kuidhinishwa kwa Mikataba husika

Kuhusiana na uidhinishaji wa mikataba husika kulingana na matakwa ya Kifungu cha 174(d) cha Ilani, Mfuko uliendelea kutoa mafao yanayoendana na matakwa ya Mkataba Namba 121 wa 1964 (Mkataba wa ajali kazini). Kwa kufanya hivyo, nchi inaweza kuridhia mkataba huu kwa urahisi kwa kuwa shughuli za Mfuko tayari zimewiana na mahitaji ya Mkataba.

### 2.8.4 Ulinzi wa Wafanyakazi

Kifungu cha 174 (c) cha Ilani ya uchaguzi kuhusu ulinzi wa wafanyakazi, Mfuko umekuwa ukitekeleza matakwa hayo kwa kuhakikisha unatoa uelewa kwa wadau kuhusu usalama na afya mahali pa kazi. Katika kipindi cha mapitio, programu za uhamasishaji zilizofanywa zilinufaisha jumla ya waajiri 1,328 na wafanyakazi 10,677 nchini kote.

### 2.8.5 Mapambano dhidi ya Ufisadi

Kwa mujibu wa Kifungu cha 11, 12, 13 na 16 cha Ilani, Mfuko umetayarisha na kuweka miongozo mbalimbali kuhusu suala hili kama vile mwongozo wa kuzuia udanganyifu na rushwa na watumishi wa Mfuko kufanyiwa uhakiki na mamlaka husika.

### 2.8.6 Maendeleo ya Viwanda

Kuhusu maendeleo ya viwanda, Mfuko unaendelea na jitihada za kufufua Kiwanda cha Chai cha Mponde kwa kushirikiana na PSSSF. Aidha, Mfuko upo katika hatua za awali za kuwekeza katika ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza vifaa tiba vitumiavyo malighafi ya pamba mkoani Simiyu kwa kushirikiana na Mfuko wa NHIF ikiwa ni utekelezaji wa Kifungu cha 33(g) cha Ilani ya Chama Tawala na Lengo la 5 la Dira ya Maendeleo 2025 (Uchumi shindani wenye uwezo wa kujenga ukuaji endelevu wenye manufaa wote). Zaidi ya hayo, shughuli za uwekezaji zinazofanywa na Mfuko husaidia kutengeneza ajira na kuchochea uchumi. Hii ni sifa muhimu ya kuimarisha ushindani wa uchumi.

### 2.8.7 Utawala Bora

Kwa mujibu wa Lengo la 3 la Dira ya Maendeleo ya 2025, Mfuko unasimamiwa na Bodi ya Wadhamini ya Utatu ambayo muundo wake umezingatia uwakilishi wa Serikali, Waajiri na Vyama vya Wafanyakazi. Aidha, Mfuko kama Taasisi nyingine zote unasimamiwa kwa kufuata sheria na kanuni za kitaifa.

## 2.9 UCHAMBUZI WA HALI

## 2.10 Uwiano wa Malengo ya Kitaifa na Mkakati wa Mfuko

Jedwali namba 2 linatoa muhtasari wa malengo ya kitaifa, hatua na jinsi Mfuko utakavyochangia katika kufikia malengo ya kitaifa kupitia Mpango Mkakati wa Mfuko.

**Jedwali 2: Mchango wa Mfuko katika kufikia Malengo ya Kitaifa**

| S/N | Malengo ya Kitaifa | Mchango wa Mfuko | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Viashiria/Vipimo | Shabaha | |
| | | | Kufikia 2021/22 | Kufikia 2026/27 |
| 1 | Kukuza tija ya kazi | Asilimia ya wafanyakazi wanaostahili na wategemezi wao waliolipwa fidia | 1 | Kukuza tija ya kazi |
| 2 | Kuboresha utoaji wa huduma | Asilimia ya matumizi ya mifumo inayojiendesha yenyewe kama njia kuu za utoaji huduma | 2 | Kuboresha utoaji wa huduma |
| 3 | Upanuzi wa wigo wa hifadhi ya jamii | Asilimia ya nguvukazi inafikiwa na Mfuko | 3 | Upanuzi wa wigo wa hifadhi ya jamii |

| S/N | Malengo ya Kitaifa | Mchango wa Mfuko | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Viashiria/Vipimo | Shabaha | |
| | | | Kufikia 2021/22 | Kufikia 2026/27 |
| 4 | Kukuza kuzuia ajali na magonjwa yanayotokana kazini | Asilimia ya uzingatiaji wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi kwa waajiri walio chini ya uangalizi | 4 | Kukuza kuzuia ajali na magonjwa yanayotokana kazini |
| 5 | Utawala na utawala wa sheria | Kiwango cha uzingatiaji kitaasisi | 5 | Utawala na utawala wa sheria |
| 6 | Uchumi imara na shindani | Uwekezaji wa fedha | 6 | Uchumi imara na shindani |

## 2.11 Hifadhi ya Jamii Tanzania Bara

Tanzania kama nchi zingine nyingi duniani inatumia Mfumo wa ILO wa nguzo tatu za usimamizi wa Programu za Hifadhi ya Jamii. Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2003 inaainisha mfumo huo wa nguzo tatu. Katika nguzo ya 1, usaidizi wa kijamii hutolewa kwa raia waliotengwa kwa sababu mbalimbali na makundi maalum. Programu kuu katika nguzo hii ni pamoja na zile zinazosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF) ambazo hutoa fedha na kazi za umma kwa maskini wanaostahili.

Nguzo ya 2 inahusu wafanyakazi walioajiriwa katika sekta rasmi. Chini ya utaratibu huu, waajiri wanalazimika kisheria kutuma michango kwa taasisi za Hifadhi ya Jamii kila mwezi. Kufikia Novemba 2021, inakadiriwa kuwa chini ya asilimia 20 ya nguvukazi inalindwa chini ya nguzo ya bima ya kijamii. Hawa ni wanachama wa Taasisi za lazima za Hifadhi ya Jamii zilizopo nchini. Taasisi hizo ni Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF).

Nguzo ya 3 inazingatia michango ya hiari iliyo juu ya mpango wa lazima. Ukiondoa WCF, mifuko mingine yote ya Hifadhi ya Jamii nchini Tanzania imetoa nafasi kwa mipango ya hiari ikizingatia mpango wa uchangiaji ulioainishwa. Kupitia chaguzi hizi, watu katika sekta isiyo rasmi wanahimizwa kuweka akiba kwa ajili ya maisha yao ya baadaye.

Licha ya juhudi hizo, bado kuna changamoto nyingi. Kwa mfano, inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 80 ya watu wa Tanzania hawahudumiwi na Mifuko ya hifadhi ya jamii. Kundi kubwa ambalo halijafikiwa na mfumo wa hifadhi ya jamii ni watu katika sekta isiyo rasmi na wakazi wa vijijini. Ni muhimu pia kusisitiza kuwa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi umeanzishwa ili kufikia malengo kadhaa ambayo ni pamoja na kuimarisha utoshelevu wa mafao ya fidia kulingana na matarajio ya Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2003 na matakwa mengine ya kisheria ikiwa ni pamoja na mikataba ya kimataifa.

## 2.12 Tathmini ya Mazingira

Mfuko ulifanya tathmini kwa dhumuni la kubaini Uwezo, Mapungufu, Fursa na Changamoto (UMFC) zinazoathiri utendaji wake. Orodha ifuatayo inatoa muhtasari wa uchambuzi wa UMFC.

### 2.12.1 Viwezeshi (Uwezo na Fursa)

(a) Uwepo wa Sheria
(b) Uwepo wa Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2003
(c) Uwepo kwa msaada wa Serikali
(d) Upatikanaji wa rasilimali za kifedha
(e) Uwepo wa Bodi ya Wadhamini
(f) Uwepo wa watumishi wenye uwezo
(g) Uwepo wa mtandao wa Watoa Huduma za Afya
(h) Uwepo wa miundombinu ya kisasa ya TEHAMA
(i) Uwepo wa mazingira mazuri ya kazi
(j) Uwepo wa taratibu za huduma zilizo wazi
(k) Ushirikiano na uhusiano na ISSA, ECASSA, TSSA na mashirika mengine
(l) yanayotoa utaalamu wa kiufundi kuhusu masuala ya hifadhi ya jamii
(m) Ushirikiano na taasisi zingine zikiwemo TRA, NBS, OSHA, NIDA, TIRA, Polisi,
(n) Tume ya Ushirika na BRELA
(o) Kuwepo kwa mifuko ya fidia iliyoendelezwa vizuri katika nchi nyingine kwa ajili
(p) ya kuchukulia mfano
(q) Uwepo wa vyombo mbalimbali vya habari nchini
(r) Kushirikiana na mifuko mingine ya hifadhi ya jamii ikiwemo miradi ya viwanda

### 2.12.2 Changamoto (Mapungufu na Vihatarishi)

(a) Uelewa mdogo kwa umma kuhusu masuala ya fidia kwa wafanyakazi
(b) Kiwango kidogo cha uwekaji wa mifumo inayojiendesha katika taratibu za
(c) utendaji kazi
(d) Uwezekano wa uwepo wa kesi
(e) Viwango vya riba vya soko visivyotabirika
(f) Uhaba wa wataalam wa masuala ya ajali mahali pa kazi katika soko la ajira
(g) Uwezekano wa kukabiliwa na matukio ya uhalifu wa kimtandao
(h) Uwezekano wa vitendo vya udanganyifu miongoni mwa waajiri, wafanyakazi
(i) na watoa huduma

### 2.12.3 Wateja na Wadau

Katika kutimiza dhima yake, Mfuko unatambua umuhimu na dhamira ya kutoa huduma bora kwa wanufaika wake muhimu na wadau kwa kutumia muda mfupi iwekekanavyo. Wadau wa Mfuko ni pamoja na Wafanyakazi, Waajiri, Serikali, Mamlaka za Udhibiti, Wakandarasi wa Uwekezaji, Benki, Wadau wa Maendeleo na Vyama vya Kitaaluma, vyombo vya habari na watoa huduma za Afya. Uchambuzi wa kina wa wadau umeonyeshwa katika **Kiambatisho cha 3**.

### 2.12.4 Pendekezo la Thamani ya Mteja

Katika kufanya tathmini ya Mfuko, wateja na wadau wengine muhimu wa Mfuko walitambuliwa na mahitaji yao kama wapokeaji wa moja kwa moja na wanufaika wa huduma za Mfuko. Hii ni hatua muhimu katika uandaaji wa Mkakati wa taasisi kwani wadau na wateja wanaweza kuwa na athari kubwa katika mafanikio au kutofanikiwa kwa taasisi. Mfuko umedhamiria kutoa fidia stahiki kwa wakati, kwa uhakika na kwa kutumia teknolojia inayofaa. Wateja na wadau wa Mfuko wameorodheshwa katika **Kiambatisho cha 2**.

## 2.13 USIMAMIZI WA VIHATARISHI

### 2.13.1 Uchambuzi wa Vihatarishi

Tathmini ya vihatarishi imefanywa ili kubaini matukio yanayoweza kuathiri Mfuko kufikia malengo yake. Taswira ya vihatarishi hubainisha asili ya kihatarishi kilichotambuliwa kulingana na uwezekano wa kutokea na athari ya kila kihatarishi mara kinapotokea. **Jedwali la 3(a) na 3(b)** linaonyesha taswira ya kihatarishi, maelezo ya kila kihatarishi, kiwango cha kihatarishi pamoja na hatua za kukabiliana nayo.

**Jedwali la 3(a):** Taswira ya Vihatarishi

| Uwezekano | Athari/matokeo | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Isiyo muhimu | Ndogo | Wastani | Kubwa | Kubwa sana |
| Karibu na Uhakika | | | 4 | | |
| Yaelekea | | | | 1,2,6,7 | |
| Yawezekana | | | 9 | | 3,8,11,13,14 |
| Isiyoelekea | | | | | 5,12 |
| Mara chache | | | | | 10 |

**Jedwali 3(b):** Tathmini ya Vihatarishi

| Na. | Maelezo ya Kihatarishi | Kiwango cha Kiha-tarishi | Hatua za Kukabiliana |
|---|---|---|---|
| 1. | Tathmini ya madai au Uhakiki wa bili za matibabu zinaweza kucheleweshwa na kusababisha malalamiko ya wateja | Juu | ♦ Mafunzo kwa Madaktari<br>♦ Kutoa mafunzo kwa wahudumu wa afya (wafanyakazi) juu ya uhakiki wa bili za matibabu<br>♦ Upelekaji wa wafanyakazi wa Sehemu ya Tathimini ya Madai katika ofisi za Mikoa za Mfuko<br>♦ Kuongeza idadi ya wafanyakazi ili kukidhi utekelezaji wa kazi zilizopo |
| 2. | Kucheleweshwa kwa Uidhinishaji wa Huduma ya Matibabu kunaweza kusababisha kuharibika kwa hadhi ya taasisi | Juu | ♦ Kutenganisha uidhinishaji wa kibali cha huduma ya matibabu katika madaraja<br>♦ Kutumia mifumo ya kidijiti katika kusimamia huduma katika Vituo vya Huduma za Afya na Watoa Huduma za Afya (HCP/HSP)<br>♦ Kutumia mifumo ya kidijiti katika kuidhin-isha matibabu |
| 3. | Ulaghai na/au rushwa unaweza kufanywa na kusababisha hasara ya kifedha na kuharibu hadhi ya taasisi | Juu | ♦ Kuimarishwa kwa udhibiti wa ndani<br>♦ Kutekeleza Sera ya Udhibiti wa Vihatarishi vya Ulaghai na Rushwa<br>♦ Kampeni ya uelimishaji kuhusu Ulaghai na Usimamizi wa Rushwa<br>♦ Kutekeleza Mkataba wa Utoaji Huduma kwa Mteja<br>♦ Kutengeneza Makubaliano ya Viwango vya Utoaji Huduma<br>♦ Kutekeleza Kanuni za Maadili ya Wafanyakazi |

| Na. | Maelezo ya Kihatarishi | Kiwango cha Kiha-tarishi | Hatua za Kukabiliana |
|---|---|---|---|
| 4. | Matarajio ya mteja yanaweza yasifikiwe na hivyo kupelekea kutoridhika na malalamiko | Juu | ♦ Kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano<br>♦ Utekelezaji wa Mkataba wa Utoaji Huduma kwa Wateja<br>♦ Kuendesha mafunzo ya huduma kwa wateja kwa Wafanyakazi wote<br>♦ Kutekeleza Programu ya elimu kuhusu taratibu za madai na nyaraka zinazohitajika<br>♦ Kutumia mfumo wa teknolojia katika Vituo vya Huduma za Afya na kwa Watoa Huduma za Afya (HCP/HSP)<br>♦ Miundombinu ya Kituo cha Simu<br>♦ Kutengeneza na kutekeleza Makubaliano ya Viwango vya Utoaji Huduma<br>♦ Kutengeneza Mfumo wa Usimamizi wa Vituo vya Huduma za Afya na Watoa Huduma za Afya (HCP/HSP). |
| 5. | Kutofuata Sheria ya Ununuzi wa Umma kunaweza kusababisha ukiukaji wa Kisheria na Usimamizi | Kati | ♦ Kuendesha mafunzo ya Sheria na Kanuni za Ununuzi kwa Bodi ya Zabuni, Idara za Watumiaji na wafanyakazi wa Kitengo cha Ununuzi<br>♦ Kutengeneza Mwongozo wa Usimamizi wa Ununuzi |
| 6. | Uchakataji wa mafao unaweza kucheleweshwa na kusababisha kutoridhika kwa mteja | Juu | ♦ Kuzingatia Mwongozo wa Usimamizi wa Madai<br>♦ Uendeshaji wa mafunzo ya uelewa juu ya taratibu za madai kwa waajiri na wafanyakazi<br>♦ Kutekeleza hatua za kisheria kwa waajiri wasiotii sheria |

| Na. | Maelezo ya Kihatarishi | Kiwango cha Kiha-tarishi | Hatua za Kukabiliana |
|---|---|---|---|
| 7. | Mchakato wa kushughulikia na kupitia madai unaweza kuchelewa na kusababisha kuharibika kwa hadhi ya taasisi | Juu | ♦ Kufanya uhakiki wa Mapato Ghafi ya Kila Mwezi ndani ya siku 15<br>♦ Kuingia katika makubaliano kati ya WCF na OSHA kuhusu masuala yanayohusiana na madai<br>♦ Kutumia mfumo wa kidijiti katika mchakato wa kupitia Madai<br>♦ Kutengeneza na kutekeleza Viwango vya Utoaji Huduma kwenye mchakato wa kupitia Madai. |
| 8. | Uhalifu wa mtandaoni unaweza kusababisha kukatizwa kwa uendeshaji wa shughuli, kuharibu hadhi ya taasisi na kupata hasara ya kifedha | Kati | ♦ Kutengeneza Sera ya Uhalifu wa Kimtandao<br>♦ Kutekeleza Kanuni za Maadili ya Wafanyakazi<br>♦ Kufanya kampeni ya kila robo mwaka ya kutoa elimu kuhusu usalama wa taarifa<br>♦ Ufungaji wa milango ya kufungua kwa kutumia alama za vidole<br>♦ Kutengeneza na kutekeleza Mkakati wa usalama wa TEHAMA<br>♦ Usajili wa wafanyakazi wasio wa idara ya TEHAMA katika rejista ya chumba cha kutunzia data<br>♦ Utekelezaji wa Sera ya Usalama wa TEHAMA<br>♦ Kutekeleza Mchakato wa kuruhusu/kufuta/kubadilisha ruhusa ya kuingia katika mifumo ya TEHAMA<br>♦ Usambazaji wa vifaa vya usalama vya Mtandao |

| Na. | Maelezo ya Kihatarishi | Kiwango cha Kiha-tarishi | Hatua za Kukabiliana |
|---|---|---|---|
| 9. | Kushindwa kwa Bodi kutekeleza majukumu yake ya uangalizi hivyo kusababisha utendaji duni wa shirika | Kati | ♦ Programu za kujenga uwezo kulingana na tathmini ya mahitaji ya mafunzo<br>♦ Mapitio ya Mkataba wa Bodi ili kuakisi viwango vya kimataifa<br>♦ Kutekeleza Kanuni za Maadili za Bodi/ Sheria ya Utumishi wa Umma<br>♦ Kutengeneza na kutekeleza kalenda ya mikutano |
| 10. | Maafa yanaweza kutokea na kusababisha kukwama kwa shughuli za uendeshaji | Chini | ♦ Kutekeleza Sera ya Kusimamia Mwendelezo wa Utendaji Kazi<br>♦ Bima ya uharibifu wa mali<br>♦ Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi kuhusu dharura na taratibu za uokoaji<br>♦ Ukaguzi wa mara kwa mara wa nyaya<br>♦ Ukaguzi wa mara kwa mara wa Vifaa vya Kuzima Moto<br>♦ Kuendesha programu ya uelimishaji wa zimamoto na uokoaji<br>♦ Upatikanaji wa umeme mbadala au jenereta<br>♦ Uwepo wa njia mbadala ya upatikanaji wa maji au hifadhi ya maji |
| 11. | Kukwama kwa shughuli za uendeshaji kunaweza kusababisha upotevu wa nyaraka na taarifa | Kati | ♦ Kutekeleza Mpango wa kurudisha mifumo ya TEHAMA baada ya majanga kutokea<br>♦ Kusimamia uzingatiaji wa Sera na Viwango vya TEHAMA<br>♦ Kutengeneza nakala rudufu ya data<br>♦ Kufanya matengenezo ya zana/vifaa mara kwa mara<br>♦ Kutumia mifumo ya kugeuza umeme<br>♦ Kutoa mafunzo kwa Wafanyakazi wa TEHAMA katika masuala ya utengenezaji wa mifumo |

| Na. | Maelezo ya Kihatarishi | Kiwango cha Kiha-tarishi | Hatua za Kukabiliana |
|---|---|---|---|
| 12. | Kutoa taarifa bila ruhusa kunaweza kusababisha uvujaji wa siri | Kati | ♦ Kutoa ruhusa maalumu kupata nyaraka katika nakala laini na nakala ngumu.<br>♦ Kutoa elimu kuhusu Utunzaji wa Nyaraka<br>♦ Mapitio ya kila mwezi ya ruhusa ya kuingia kwenye mfumo<br>♦ Utatuzi na urekebishaji wa changamoto za TEHAMA kufanywa kwa wakati<br>♦ Uanzishaji wa Masijala ya siri |
| 13. | Taarifa za madai zinaweza kuwa sio sahihi na kusababisha kuharibika kwa hadhi ya taasisi na upotevu wa fedha | Kati | ♦ Kutekeleza Mwongozo wa Usimamizi wa Madai<br>♦ Kutumia mifumo ya kidijiti katika usimamizi wa Vituo vya Huduma za Afya na Watoa Huduma za Afya (HCP/HSP)<br>♦ Kutoa mafunzo ya uchunguzi wa madai ili kuboresha ubora wa uchunguzi |
| 14. | Kutofuata Sheria, Kanuni, Miongozo na Maagizo ya Serikali, Bodi na Menejimenti kunaweza kusababisha hasara ya kifedha na kuharibika kwa hadhi ya taasisi. | Kati | ♦ Kutengeneza mwongozo wa uzingatiaji wa kitaasisi<br>♦ Kuhakikisha uhudhuriaji katika warsha za kitaalamu na usimamizi |

# SURA YA TATU

## 3.0 MKAKATI WA MFUKO

### 3.1 Pendekezo la Thamani ya Mteja

Thamani ya wateja na wadau inatafsiri mahitaji ya wateja na wadau katika Mkakati wa Mfuko. Pendekezo la thamani ni thamani maalumu ya ziada ambayo Mfuko itatoa kwa wateja wake kupitia shughuli zake. Jedwali hili linaeleza kwa ufupi ahadi ya thamani kwa mteja inayotolewa na Mfuko kuzidi matarajio ya mteja.

| **WATEJA NA WADAU** | **BIDHAA NA HUDUMA**<br>Bidhaa na huduma ambazo Mfuko inatoa zina sifa zifuatazo: | **TASWIRA**<br>Taswira ambayo Mfuko unapenda kuionesha ina sifa zifuatazo: | **UHUSIANO**<br>Uhusiano ambao Mfuko unapenda kuwa nao kati yake na wateja pamoja na wadau unaweza kuelezwa hivi: |
|---|---|---|---|
| ♦ Wanachama<br>♦ Waajiri<br>♦ Familia<br>♦ Jamii<br>♦ Serikali | ♦ Huduma za kuaminika<br>♦ Fidia Toshelevu<br>♦ Huduma kwa wakati<br>♦ Inayookoa gharama<br>♦ Zinazoendeshwa kidijiti<br>♦ Mteja kipaumbele | ♦ Usahihi<br>♦ Uwazi<br>♦ Uaminifu<br>♦ Uwajibikaji | ♦ Kujali<br>♦ Usawa<br>♦ Usikivu<br>♦ Usiopendelea |

### 3.2 Maeneo ya Vipaumbele

Katika mchakato wa kuchagua mwelekeo wa mkakati, faida na hasara za mikakati mbadala zilitathminiwa. Jedwali mkakati hapa linaakisi kielelezo cha picha cha msisitizo ambao mkakati wa Mfuko umeweka kwenye mambo muhimu au vitu vitakavyoongoza utendaji. Grafu ya mkakati inaonesha namna mkakati wa Mfuko umejiweka sambamba na dhumuni la kimkakati. Ulinganifu unachagiza mazungumzo katika vitendo vitakavyozalisha gharama mkakati upya katika kutoa huduma kwa wanufaika.

Mchanganuo wa mkakati ufuatao unatambulisha Vichocheo vya Ukuaji kama kufungua matawi na uwekezaji wa mtaji wa rasilimali watu na Vichocheo vya Kifedha kama kukua kwa uwekezaji na ukusanyaji wa michango wakati Vichocheo vya Ufanisi ni uwekezaji katika teknolojia na kuimarisha uboreshaji wa huduma.

(a) **Kuimarisha Mtandao wa Matawi**

Juhudi kubwa zitawekwa kuhakikisha kuwa mtandao wa matawi ya mikoa wa Mfuko unaboreshwa kwa ajili ya kutoa huduma kwa ufanisi, kuleta urahisi kwa wanufaika na wadau kufikia huduma na kuimarisha utekelezaji wa utaratibu.

(b) **Kuendeleza Mtaji wa Rasilimali watu**

Mfuko utaongeza juhudi katika kuimarisha ujuzi na utaalamu wa watumishi kwa kuziba ombwe la ujuzi, kuimarisha weledi wa taasisi na wa watumishi, kujenga utamaduni unaofaa wa taasisi, kuhakikisha watumishi wanaziishi tunu za taasisi, kuweka nguvu katika mpango wa kurithishana na kuimarisha ustawi na maendeleo ya watumishi. Matarajio ya Mfuko ni kuendeleza watumishi wenye utii na unyenyekevu wakati wote katika kuendeleza dira ya Mfuko.

(c) **Kufanya Uwekezaji kwa Umakini**

Katika kuhakikisha kuwa Mfuko unaendelea kuwa himilivu, kanuni za uwekezaji, miongozo na sera zitafuatwa. Hii itawezesha kuwepo kwa usalama katika uwekezaji, mapato makubwa, ukwasi wa kiwango cha juu, mchanganyiko katika jedwali la uwekezaji ambao kwa pamoja unatoa manufaa ya juu kiuchumi na kijamii.

(d) **Kukuza Ukusanyaji Michango**

Mfuko utajikita kujihusisha na wadau mbalimbali kuwezesha ukusanyaji wa michango ili kuwezesha ulipaji stahiki wa mafao. Mfuko utahamasisha kujitolea kwa wadau katika kufuata sheria kupitia elimu na ushirikishwaji wa waajiri.

(e) **Uwekezaji katika Teknolojia ya Kisasa**

Mfuko utawezesha matumizi ya teknolojia ya kisasa ili kujiweka sambamba na mabadiliko ya mara kwa mara ya teknolojia na mazingira ambako taasisi inafanyia kazi katika kutoa huduma bora. Hii ni pamoja na mifumo ya utendaji kazi kwa njia ya kidijiti na kutengeneza mifumo mingine ya TEHAMA ili kuwarahisishia watumishi, waajiri na watoa huduma kuwasiliana na Mfuko.

(f) **Kuimarisha Huduma Bora**

Mfuko utawekeza katika kuboresha huduma zake ili kuongeza kiwango cha kuridhika kwa wateja kupitia utoaji wa huduma za haraka, sahihi, zinazoaminika na zinazomlenga mteja.

Taarifa zaidi ya maeneo ya vipaumbele vya Mfuko zinaoneshwa katika jedwali mkakati hapa chini.

**Kielelezo cha 20:** Hali ya kimkakati




## 3.3 Maeneo Makuu na Matokeo ya Kimkakati ya Mfuko

Katika kutengeneza mkakati, Mfuko umeainisha maeneo makuu manne yanayobainisha vipaumbele ya mkakati wake. Haya ni maeneo muhimu ambayo Mfuko utajiimarisha katika kufikia dhima, dira na mkakati wake na yanatambuliwa kama "Nguzo za Ubora". Maeneo hayo ya kimkakati ni Kuwajali Wateja, uendelevu wa kifedha, utendaji bora na Ushirikiano wa kimkakati.




Kielelezo hapa chini kinaonesha maeneo mkakati manne na matokeo yanayohusiana nayo:

## 3.4 Mitazamo

Mitazamo ya Kimkakati ni lenzi ambazo Mfuko unatazama utendaji wake. Mitazamo hiyo inatumika kujumuisha shughuli za Mfuko. Mfumo wa uendeshaji wa Mfuko, ambao unaojumuisha dhima, dira na mkakati, unabainisha maeneo makuu ya kimtazamo. Mitazamo ya Mfuko imeelezwa katika mchoro ufuatao.

**Mtazamo wa wateja**: Tunawezaje kuongeza thamani ya wateja na

**Mtazamo wa usimamizi wa fedha**: Tunawezaje kuongeza thamani ya wadau ili kuweza kuifikia dhima ya taasisi kwa ufanisi

**Mtazamo wa mifumo ya ndani ya utendaji kazi**: Kufikia matarajio ya wateja na wadau wetu ni mchakato gani katika utoaji wa huduma unapaswa kuboreshwa

**Mtazamo wa kujifunza na ukuaji**: Kufikia ufanisi wa taratibu za utoaji huduma, Ni uwezo upi taasisi yetu inahitaji kuwa nao na kuuboresha

## 3.5 Malengo Mkakati

Jumla ya malengo mkakati saba (7) yameandaliwa kuwezesha Mfuko kutimiza dhima yake ya *"Kutoa huduma stahiki za fidia kwa wafanyakazi ambazo zitapunguza athari za kijamii na kiuchumi zitokanazo na ajali pamoja na magonjwa yatokanayo na kazi"* na kutimiza dira yake ya "*Mfano wa kuigwa katika utoaji wa huduma za fidia kwa wafanyakazi barani Afrika*". Malengo mkakati ya Mfuko yaligawanywa katika maeneo makuu manne ya mfumo wa kupanga matokeo. Malengo mkakati haya ndiyo msingi katika mkakati na yataainisha utekelezaji wa malengo mkakati katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

### 3.5.1 Malengo Mkakati, Maelezo na Matokeo Tarajiwa

| *Lengo Mkakati* | *Maelezo na Matokeo Tarajiwa* |
|---|---|
| MTAZAMO WA WATEJA NA WADAU | |
| 1. *Kuongeza kiwango cha kuridhika kwa wateja na wadau* | **Maelezo**<br>Lengo hili linakusudia kuhakikisha kuwa Mfuko unakuwa na tija kwa wateja wake kwa kutoa huduma bora za kiwango cha juu cha kuaminika na kwa wakati. Mfuko utaendelea kuboresha huduma na kutoa mrejesho unaotakiwa kwa wateja wake. Mfuko utawashirikisha wateja kupitia mikutano mbalimbali ikiwemo mkutano wa mwaka wa wadau, huduma za mtandaoni za moja kwa moja, kituo cha mawasiliano, kufanya tafiti za kupima kuridhika kwa mteja ili kujenga uelewa wa taswira ya taasisi.<br><br>**Matokeo Tarajiwa**<br>♦ Kuongeza kiwango cha kuridhika kwa wanachama (wanufaika, waajiri, wafanyakazi)<br>♦ Kuongeza kiwango cha kuridhika kwa wadau (wategemezi, wasimamizi, serikali) |

| MTAZAMO WA KIFEDHA | |
|---|---|
| 2. *Kuimarisha Ustahimilivu wa Kifedha* | **Maelezo**<br><br>Lengo hili linakusudia kuendeleza ukuaji wa kifedha wa Mfuko utakaowezesha kutoa huduma endelevu. Mfuko utaboresha ukuaji wake pamoja na mambo mengine; kwa njia ya makusanyo ya michango kutoka kwa waajiri, usimamizi wa rasilimali fedha na kufanya uwekezaji kwa umakini.<br><br>**Matokeo Tarajiwa**<br>♦ Ukuaji katika uwekezaji<br>♦ Faida kubwa kutokana na uwekezaji<br>♦ Kuongezeka kwa makusanyo ya michango<br>♦ Akiba toshelevu |
| MTAZAMO WA MIFUMO YA UTENDAJI KAZI | |
| 3. *Kuboresha Ufanisi katika utendaji* | **Maelezo**<br><br>Lengo hili linakusudia kuimarisha utoaji wa huduma kwa kujihakikishia kuwa muda wa uchakataji wa malipo unapunguzwa, shughuli hazikwamishwi, umakini unaongezeka, makosa na marudio ya kazi yanapunguzwa. Hii inamaanisha pia kuwa shughuli zote za utendaji kazi ndani ya Mfuko zinafikia viwango stahiki vya utoaji huduma na uendeshaji.<br><br>**Matokeo Tarajiwa**<br>♦ Kupunguza muda wa utoaji huduma<br>♦ Makosa kupungua<br>♦ Kuzingatia viwango |
| 4. *Kuimarisha Utii wa Sheria* | **Maelezo**<br><br>Lengo hili linakusudia kuhakikisha Mfuko unaimarisha usajili wa waajiri ili kuongeza idadi ya waajiri wanaochangia na wanufaika, ulipaji michango kwa wakati na uzingatiaji wa viwango vya afya na usalama mahali pa kazi.<br><br>**Matokeo tarajiwa**<br>♦ Utii wa sheria kwa Waajiri<br>♦ Kuongezeka kwa waajiri wanaochangia<br>♦ Kupungua kwa ajali na magonjwa yatokanayo na kazi |

| MTAZAMO WA KUJIFUNZA NA UKUAJI | |
|---|---|
| 5. *Kuimarisha Utawala* | **Maelezo**<br><br>Lengo hili lina nia ya kuhakikisha kuwa Mfuko una muundo wa uongozi na utawala wa Bodi iliyo hai, sera na miongozo inayoendana na wakati, utendaji unaozingatia sheria na unaowajibika kwa matokeo ya vitendo vyake.<br><br>**Matokeo Tarajiwa**<br><br>♦ Vihatarishi vilivyo katika hali ya kustahimilika<br>♦ Kuongezeka kwa utii wa sheria<br>♦ Kuongezeka kwa uwajibikaji |
| 6. *Kuboresha teknolojia* | **Maelezo**<br><br>Mfuko utatumia teknolojia ya kisasa kukabiliana na mahitaji ya mabadiliko ya haraka katika teknolojia kuweza kuwa katika mazingira hayo. Hili linamaanisha kuwa watumishi watapata fursa ya kupata na kuitumia teknolojia kuboresha utendaji katika vitengo vyao.<br><br>**Matokeo Tarajiwa**<br><br>♦ Kupungua kwa ombwe la teknolojia<br>♦ Matumizi bora ya teknolojia<br>♦ Utatuzi wa changamoto kwa kutumia ubunifu |
| 7. *Kuboresha uwezo wa watumishi* | **Maelezo**<br><br>Lengo hili limejikita kuongeza utumishi wenye tija katika Mfuko kupitia programu za kuendeleza ujuzi na usimamizi wa maarifa. Mfuko utaboresha weledi wa watumishi wake kwa kuwawekea fursa za kuendelea kujifunza, kuunganisha programu za kujiendeleza na mafunzo na njia za kujiendeleza kikazi na kurithishana, kupata uzoefu kutumia wataalamu mbalimbali ili kufikia malengo mkakati ya Mfuko. Lengo litajumuisha pia kuwasaidia watumishi katika masuala ya afya ya mwili, kihisia, kisaikolojia, kiroho na ustawi kifedha.<br><br>**Matokeo tarajiwa**<br><br>♦ Watumishi wenye ujuzi na weledi<br>♦ Utendaji kazi wenye tija kutoka kwa watumishi<br>♦ Watumishi wengi wenye uwezo wa uongozi<br>♦ Watumishi wengi wenye utendaji uliovuka malengo |

## 3.6 Ramani Mkakati

Ramani mkakati ya Mfuko ni kielelezo cha mwonekano wa namna taasisi itakavyoboresha huduma kwa wateja na wadau wote. Pia ramani mkakati inaonesha mahusiano baina ya malengo mkakati katika kuleta tija kwa mteja.

**Kielelezo cha 1:** Ramani Mkakati




## 3.7 Ahadi ya Mfuko katika kutoa tija kwa Wadau

Kama Mfuko, lengo letu ni "*Kutoa Huduma za Fidia za Kuaminika na Fanisi kwa Wafanyakazi zitakazowawezesha kukabiliana na Athari za Kijamii na Kiuchumi zinazotokana na ajali na magonjwa mahali pa Kazi*" na dira yetu ni "*Mfano wa Kuigwa katika Utoaji wa Huduma za Fidia kwa Wafanyakazi barani Afrika*". Kufikiwa kwa dira hii kunategemea na utekelezwaji wa mikakati minne ambayo ni: Uhusiano wa Kimkakati, Uendelevu wa Kifedha, Kuwajali Wateja na Ubora katika Utendaji.

Mafanikio yetu yatatafsiriwa kwa kiwango cha kuridhika kwa wateja na wadau wetu (1) kupitia uendelevu wa kifedha (2) na ubora katika utendaji (3). Mafanikio yetu ya kifedha yatachagizwa na uwezo wetu wa kuimarisha uzingatiaji (4) na nidhamu ya matumizi, huku uwezo wetu wa kujifunza na kukua kupitia kuimarisha utawala (5), kuboresha teknolojia (6) na kuimarisha uwezo wa wafanyakazi (7) ukiwa ni msingi utakaoongeza ufanisi wa mifumo ya utendaji kazi.

Kama taasisi ya umma, tunaweka msisitizo katika kujenga utamaduni wezeshi wa shirika, na msingi imara wa utawala ikiwa ni nguzo muhimu ya uwezo wa ndani na kwa kupitia jitihada hizi tutaleta maboresho katika ufanisi wa utendaji kazi.

Kwa ujumla, mafanikio ya utekelezaji wa mipango yetu na kufikia malengo mkakati yatategemea misingi mitatu: *Uongozi shirikishi katika ngazi zote, mawasiliano ya pande mbili na kudumisha tunu za Mfuko – Uadilifu, Umahiri, Ushirikiano, Uwajibikaji na kujali.*

## 3.8 Vipimo vya Utendaji

Vipimo vya utendaji kwa kila lengo la mkakati viliwekwa ili kuwezesha uchambuzi katika kufanya maamuzi na kuweka mkazo katika mambo ya msingi zaidi. Vipimo vya utendaji vilivyoorodheshwa katika jedwali linalofuata viliandaliwa kwa ajili ya kufanya tathmini ya ufanisi wa utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Mfuko kwa miaka mitano ijayo.

### 3.8.1 Vipimo vya Utekelezaji wa Malengo Mkakati

| LENGO MKAKATI | VIPIMO VYA UTENDAJI | |
|---|---|---|
| **MTAZAMO WA WATEJA** | | **SHABAHA** |
| **1. Kuongeza kiwango cha kuridhika kwa Mwanachama na Wadau** | ♦ Kiwango cha kuridhika kwa wanachama<br>♦ Asilimia ya malalamiko ya wateja yaliyoshughulikiwa kwa wakati<br>♦ Kiwango cha kuridhika kwa wadau<br>♦ Kiwango cha kufahamika kwa Mfuko | ♦ 90%<br>♦ 90%<br>♦ 80%<br>♦ 90% |
| **MTAZAMO WA KIFEDHA** | | |
| **2. Kuimarisha Uwezo Endelevu wa Kifedha** | ♦ Asilimia ya ufanisi wa makusanyo ya michango iliyowekwa katika bajeti<br>♦ Uwiano wa rasilimali na dhima ya mafao<br>♦ Mapato halisi ya uwekezaji<br>♦ Gharama za uendeshaji: Jumla ya mapato | ♦ 95%<br>♦<br>♦ 1.2<br>♦<br>♦ 3%<br>♦ 20% |
| **MTAZAMO WA MIFUMO YA UTENDAJI KAZI** | | |
| **3. Kuboresha Utendaji Kazi** | ♦ Kiwango cha utekelezaji wa hati ya mkataba wa utoaji huduma kwa mteja<br>♦ Kiwango cha utekelezaji wa makubaliano ya utoaji huduma<br>♦ Asilimia ya madai yaliyolipwa ndani ya muda | ♦ 95%<br>♦ 100%<br>♦ 90% |

| LENGO MKAKATI | VIPIMO VYA UTENDAJI | |
|---|---|---|
| **MTAZAMO WA WATEJA** | | **SHABAHA** |
| **4. Kuimarisha Uzingatiaji** | ♦ Kiwango cha uzingatiaji wa waajiri katika kulipa michango<br>♦ Asilimia ya uzingatiaji katika kujisajili kwa waajiri<br>♦ Asilimia ya kupungua kwa ajali na magonjwa yatokanayo na kazi | ♦ 95%<br>♦<br>♦ 95%<br>♦<br>♦ 10%<br>♦ |
| **MTAZAMO WA KUJIFUNZA NA UKUAJI** | | |
| **5. Kuimarisha Utawala** | ♦ Kielezo cha vihatarishi<br>♦ Hati ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali<br>♦ Kiwango cha uzingatiaji wa matakwa ya wadhibiti<br>♦ Uzingatiaji wa taasisi | ♦ <20%<br>♦ Safi<br>♦ 86%<br>♦ 97% |
| **6. Kuboresha Teknolojia** | ♦ Kiwango cha ombwe la teknolojia<br>♦ Kiwango cha kutumia teknolojia | ♦ <30%<br>♦ 80% |
| **7. Kuimarisha Uwezo wa Wafanyakazi** | ♦ Kiwango cha ombwe la ujuzi<br>♦ Kiwango cha uzalishaji wa wafanyakazi<br>♦ Kiwango cha kurithishana madaraka<br>♦ Kiwango cha kuridhika kwa wafanyakazi | ♦ <10%<br>♦ 90%<br>♦<br>♦ 80%<br>♦<br>♦ 80% |

## 3.9 Shughuli Mkakati

Mfuko umeainisha programu au miradi maalumu ambayo utekelezaji wake utawezesha utekelezaji wa mkakati na kusaidia ufanyaji wa maamuzi na uwekaji wa vipaumbele vya miradi kulingana na matokeo yake ya kimkakati. Shughuli hizi zimeainishwa katika Jedwali hapa chini kuonyesha matokeo yake katika malengo ya mkakati ya Mfuko.

| | SHUGHULI MKAKATI | MALENGO YA KIMKAKATI YANAYOATHIRIWA | | | | | | | | NAMBA YA UTAMBULISHO WA LENGO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | CS1 | FS1 | BP1 | BP2 | LG1 | LG2 | LG3 | # | |
| 1 | Andaa na kutekeleza mpango wa menejimenti ya vitegauchumi vya uwekezaji | | | | | | | | 3 | CS1:Kuongeza kiwango cha kuridhika kwa Wanachama na Wadau |
| 2 | Andaa na kutekeleza Mpango wa menejimenti ya ubora wa huduma | | | | | | | | 4 | FS1: Kuimarisha uwezo endelevu wa kifedha |
| 3 | Andaa na kutekeleza Mkakati wa kuzuia ajali na magonjwa yatokanayo na kazi | | | | | | | | 3 | |
| 4 | Andaa na kutekeleza program za kukuza uzingatiaji miongoni mwa waajiri | | | | | | | | 5 | IBP1: Kuboresha Utendaji Kazi |
| 5 | Andaa na kutekeleza mpango wa maboresho ya mfumo wa utendaji kazi | | | | | | | | 6 | |
| 6 | Andaa na kutekeleza mkakati wa utoaji wa huduma za TEHAMA | | | | | | | | 7 | IBP2: Kuimarisha Uzingatiaji |
| 7 | Andaa na kutekeleza mpango wa uendelezwaji wa rasilimali watu | | | | | | | | 7 | |
| 8 | Andaa na kutekeleza mpango wa ushirikiano wa kimkakati | | | | | | | | 7 | L&G1: Kuimarisha Utawala |
| 9 | Andaa na kutekeleza program za ustawi wa wafanyakazi | | | | | | | | 5 | |
| 10 | Andaa na kutekeleza mpango wa mawasiliano na mabadiliko | | | | | | | | 5 | L&G2: Kuboresha Teknolojia |
| 11 | Andaa na kutekeleza mpango wa menejimenti ya rasilimali fedha | | | | | | | | 4 | |
| 12 | Andaa na kutekeleza mkakati wa utengemao | | | | | | | | 5 | L&G3: Kuimarisha Uwezo wa Wafanyakazi |
| 13 | Fanya mapitio ya sheria na mazingira ya usimamizi | | | | | | | | 5 | |

Mfuko umeandaa shughuli mkakati 13 kama miradi mahususi ambayo itatekelezwa ili kutekeleza mkakati wa Mfuko na kufikia dira yake. Shughuli hizi zilipewa kipaumbele ili kuhakikisha Mfuko unapata mafanikio ya haraka na kuleta tija. Katika kuweka vipaumbele vya shughuli, matokeo ya kimkakati na kiwango cha rasilimali zinazohitajika vilizingatiwa. Shughuli zenye matokeo makubwa ya kimkakati na gharama ndogo zilichaguliwa kama kipaumbele katika utekelezaji ambapo zile zenye matokeo makubwa ya kimkakati na zenye uhitaji mkubwa wa rasilimali zitahitaji mipango ya muda mrefu ili kuleta mafanikio ya muda mrefu. Mchoro hapo chini unaonesha mgawanyo wa shughuli mkakati za Mfuko.




## 3.10 Upimaji wa Malengo ya Mpango Mkakati wa Mfuko

Kutoa elimu kuhusu mpango ni nyenzo muhimu ya kuweka taswira ya taasisi kwenye mpango. Mchoro wa mpango mkakati unaonesha mambo muhimu ya kimkakati yaliyoandaliwa katika namna rahisi inayoeleweka. Kadi ya matokeo ya mfuko, inayoonesha jinsi mtiririko wa thamani ulivyoainishwa katika muhtasari wa mkakati wa Mfuko kwa namna inavyoweza kutumika na kusomeka kirahisi, imeoneshwa hapa chini.

# MFUKO WA FIDIA KWA WAFANYAKAZI
# MPANGO MKAKATI & MFUMO WA UPIMAJI WA MALENGO

| DIRA | DHIMA | | TUNU |
|---|---|---|---|
| *Mfano wa kuigwa katika utoaji wa huduma za fidia kwa wafanyakazi barani Afrika* | *Kutoa Huduma Stahiki za Fidia na kwa Ufanisi Zinazokabiliana na Athari za Kijamii na Kiuchumi Zitokanazo na Ajali na Magonjwa yatokanayo na Kazi.* | | Uadilifu, Umahiri, Ushirikiano, Uwajibikaji na Kujali |
| **STRATEGIC THEMES & THEME RESULTS** | | | |
| KUMJALI MTEJA<br>***Matokeo Mkakati:***<br>Kiwango cha kuridhika kwa mteja kwa 90% kufikia 2027 | UHUSIANO WA KIMKAKATI<br>***Matokeo Mkakati:***<br>*Kuongezeka kwa tija kwa Mfuko kupitia ushirika wenye thamani kwa Mfuko* | UENDELEVU WA KIFEDHA<br>***Matokeo Mkakati:***<br>Fikia uwiano wa rasilimali na dhima ya mafao wa 1.2 kufikia 2027 | UBORA KATIKA UTENDAJI<br>***Matokeo Mkakati:***<br>*Wanachama wahudumiwe kwa haraka, kwa umahiri na huruma kupitia utoaji wa huduma bora* |

## WCF RAMANI MKAKATI




| LENGO LA MKAKATI | KIPIMIO CHA KIMKAKATI | |
|---|---|---|
| Mtazamo: Wateja | Kipimio | Shabaha |
| 1 Kuongeza kiwango cha kuridhika kwa Mwanachama na Wadau | • Kiwango cha kuridhika kwa mteja<br>• % ya malalamiko ya wateja yaliyoshughulikiwa kwa wakati<br>• Kiwango cha kufahamika kwa Mfuko | • 90%<br>• 90%<br>• 80%<br>• 20% |
| **Mtazamo: Kifedha** | | |
| 2. Kuimarisha uwezo endelevu wa Kifedha | • % ya ufanisi wa makusanyo ya bajeti ya michango<br>• Uwiano wa rasilimali na dhima ya mafao<br>• Mapato ya uwekezaji<br>• Gharama za uendeshaji: Jumla ya mapato | • 95%<br>• 1.2<br>• 3%<br>• 20% |
| **Mtazamo: Mifumo ya Utendaji Kazi** | | |
| 3. Kuboresha Utendaji Kazi | • Kiwango cha utekelezaji wa hati ya mkataba wa utoaji huduma kwa mteja<br>• Kiwango cha utekelezaji wa makubaliano ya utoaji huduma<br>• % ya madai yaliyolipwa ndani ya muda | • 95%<br>• 100%<br>• 90% |
| 4. Kuimarisha Uzingatiaji | • Kiwango cha uzingatiaji wa kulipa michango cha waajiri<br>• % ya uzingatiaji wa kujisajili kwa waajiri<br>• % ya kupungua kwa ajali na magonjwa mahali pa kazi<br>• % ya uzingatiwaji wa afya na usalama mahali pa kazi kwa waajiri walioainishwa | • 95%<br>• 95%<br>• 10%<br>• 80% |
| **Mtazamo: Kujifunza na Ukuaji** | | |
| 5. Kuimarisha Utawala | • Kielezo cha vihatarishi<br>• Hati ya Mkaguzi na Mdhibiti wa hesabu za serikali<br>• Kiwango cha uzingatiwaji wa matakwa ya wadhibiti<br>• Uzingatiaji wa taasisi | • <20%<br>• Safi<br>• 86%<br>• 97% |
| 6. Kuboresha Teknolojia | • Upungufu katika teknolojia<br>• Kiwango cha kutumia teknologia | • 30%<br>• 80% |
| 7. Kuimarisha Uwezo wa Wafanyakazi | • Upungufu wa ujuzi<br>• Kiwango cha uzalishaji cha wafanyakazi<br>• Kiwango cha kurithishana majukumu<br>• Kiwango cha kuridhika kwa wafanyakazi | • 10%<br>• 90%<br>• 80%<br>• 80% |

### SHUGHULI MKAKATI

1) Andaa na kutekeleza program za utawala na uwajibikaji
2) Andaa na kutekeleza mpango wa menejimenti ya vitega uchumi vya uwekezaji
3) Andaa na kutekeleza Mpango wa menejimenti ya ubora wa huduma
4) Andaa na kutekeleza Mkakati wa kuzuia ajali na magonjwa yatokanayo na kazi
5) Andaa na kutekeleza program za kukuza uzingatiaji miongoni mwa waajiri
6) Andaa na kutekeleza mpango wa maboresho ya mfumo wa utendaji kazi
7) Andaa na kutekeleza mkakati wa utoaji wa huduma za TEHAMA
8) Andaa na kutekeleza mpango wa uendelezwaji wa rasilimali watu
9) Andaa na kutekeleza mpango wa ushirikiano wa kimkakati
10) Andaa na kutekeleza program za ustawi wa wafanyakazi
11) Andaa na kutekeleza mpango wa mawasiliano na mabadiliko
12) Andaa na kutekeleza mpango wa menejimenti ya rasilimali fedha
13) Andaa na kutekeleza mkakati wa utengemao

**Jedwali 6: Kuunganisha Majukumu ya Msingi na Malengo Mkakati**

| SN | Majukumu ya Msingi kwa mujibu wa Sheria | Malengo yanayoendana na Mpango Mkakati |
|---|---|---|
| **1.** | Kulipa fidia stahiki na toshelevu | 1. Kuongeza kiwango cha kuridhika kwa Mwanachama na Wadau<br>2. Kuimarisha uwezo endelevu wa Kifedha<br>3. Kuboresha Utendaji Kazi<br>4. Kuimarisha Uzingatiaji<br>5. Kuimarisha Utawala<br>6. Kuboresha Teknolojia<br>7. Kuimarisha Uwezo wa Wafanyakazi |
| **2.** | Kutekeleza Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2003 iliyoweka matakwa ya uwepo wa utaratibu wa fidia kwa wafanyakazi pale mfanyakazi atakapoumia, kuugua ama kufariki dunia kutokana na kazi | 1. Kuongeza kiwango cha kuridhika kwa Mwanachama na Wadau<br>2. Kuimarisha uwezo endelevu wa Kifedha<br>3. Kuboresha Utendaji Kazi<br>4. Kuboresha Teknolojia |
| **3.** | Kutekeleza matakwa ya kifungu cha 5 cha Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi | 1. Kuongeza kiwango cha kuridhika kwa Mwanachama na Wadau<br>2. Kuimarisha uwezo endelevu wa Kifedha<br>3. Kuboresha Utendaji Kazi<br>4. Kuimarisha Uzingatiaji<br>5. Kuimarisha Utawala<br>6. Kuboresha Teknolojia<br>7. Kuimarisha Uwezo wa Wafanyakazi |
| **4.** | Kuweka utaratibu utakaowezesha kuharakisha malipo ya fidia kwa wafanyakazi ama wategemezi wao | 1. Kuongeza kiwango cha kuridhika kwa Mwanachama na Wadau<br>2. Kuimarisha uwezo endelevu wa Kifedha<br>3. Kuboresha Utendaji Kazi<br>4. Kuimarisha Utawala<br>5. Kuboresha Teknolojia<br>6. Kuimarisha Uwezo wa Wafanyakazi |

| SN | Majukumu ya Msingi kwa mujibu wa Sheria | Malengo yanayoendana na Mpango Mkakati |
|---|---|---|
| **5.** | Kuweka utaratibu utakaowezesha Mfuko kupokea michango kutoka kwa waajiri na kufanya malipo | 1. Kuongeza kiwango cha kuridhika kwa Mwanachama na Wadau<br>2. Kuimarisha uwezo endelevu wa Kifedha<br>3. Kuboresha Utendaji Kazi<br>4. Kuimarisha Utawala<br>5. Kuboresha Teknolojia<br>6. Kuimarisha Uwezo wa Wafanyakazi |
| **6.** | Kukuza mbinu za kuzuia ajali na magonjwa yanayotokana na kazi | 1. Kuongeza kiwango cha kuridhika kwa Mwanachama na Wadau<br>2. Kuimarisha uwezo endelevu wa Kifedha<br>3. Kuimarisha Uzingatiaji<br>4. Kuimarisha Uwezo wa Wafanyakazi |
| **7.** | Kutoa huduma za utengemao | 1. Kuongeza kiwango cha kuridhika kwa Mwanachama na Wadau<br>2. Kuimarisha uwezo endelevu wa Kifedha<br>3. Kuboresha Teknolojia<br>4. Kuimarisha Uwezo wa Wafanyakazi |
| **8.** | Kukidhi matakwa ya mikataba ya kimataifa kuhusu fidia kwa wafanyakazi | 1. Kuongeza kiwango cha kuridhika kwa Mwanachama na Wadau<br>2. Kuimarisha uwezo endelevu wa Kifedha<br>3. Kuboresha Utendaji Kazi<br>4. Kuimarisha Uzingatiaji<br>5. Kuimarisha Utawala<br>6. Kuboresha Teknolojia |

# SURA YA NNE

## 4.0 MPANGO WA KIFEDHA

### 4.1 Utangulizi

Sura hii inaonesha makisio ya rasilimali fedha ambazo zitakusanywa na kutumika katika kutekeleza Mpango Mkakati huu. Kwa hali hii, makisio ya mapato na matumizi yameainishwa. Aidha, nadharia zilizotumika katika kuandaa makisio husika zimeoneshwa.

### 4.2 Nadharia za kiuchumi

Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, uchumi ulikuwa kwa wastani wa 6.24% kwa mwaka. Katika kipindi cha mpango huu, ukuaji wa uchumi unakadiriwa kuwa wa 8.0% kufikia mwezi Juni 2027. Katika uandaaji wa makisio haya, Mfuko ulizingatia vigezo vingine vya ukuaji wa uchumi ambavyo vinategemewa kuendelea kuwa imara. Vigezo vilivyozingatiwa ni pamoja na mfumuko wa bei, riba na thamani ya fedha ukilinganisha na fedha za kigeni.

#### 4.2.1 Dhana Muhimu

Dhana zifuatazo zilitumika katika uandaaji wa makisio ya mapato na matumizi ya Mfuko katika kipindi cha Mpango Mkakati huu:

(a) Vyanzo vikuu vya mapato ni michango ya waajiri, mapato ya uwekezaji pamoja na mapato mengine;

(b) Asilimia 100 ya mapato yanayosalia baada ya matumizi itawekezwa kila mwaka;

(c) Kwa kupitia uimarishaji wa ofisi za mikoa, matumizi ya teknolojia stahiki, kuongezeka kwa shughuli za ukaguzi, utambuzi wa waajiri wapya na elimu kwa umma, inatarajiwa kwamba Mfuko utakuwa umesajili asilimia 95 ya waajiri wote ifikapo tarehe 30 Juni 2027;

(d) Michango ya waajiri inategemea kuongezeka kufikia Shilingi bilioni 116.40 kufikia Juni 2027 ikiwa ni matokeo ya kuimarishwa kwa ofisi za mikoa, kuongezeka kwa shughuli za ukaguzi, usajili wa waajiri wapya, nyongeza ya mishahara na kuongezeka kwa elimu kwa umma;

(e) Kiwango cha uchangiaji kitakuwa ni asilimia 0.5 na 0.6 ya mapato ghafi ya wafanyakazi wa sekta ya umma na binafsi mtawalia;

(f) Kiwango cha chini cha mapato halisi ya uwekezaji kinatarajiwa kuwa asilimia 3 kwa mwaka wakati wa utekelezaji wa mpango huu; na

(g) Gharama za uendeshaji wa shughuli za Mfuko dhidi ya mapato inatarajiwa kuwa asilimia 19.50 katika kipindi cha utekelezaji wa mpango huu. Aidha, makadirio yanaonesha kuwa kiwango hicho cha gharama za uendeshaji wa shughuli za Mfuko kitazidi asilimia 15 iliyowekwa kwa mujibu wa kifungu 84(2) cha Sheria. Mfuko utatumia kifungu cha 84(2) cha Sheria kuomba idhini ya kuendelea na matumizi hayo. Muhtasari wa gharama za uendeshaji ni kama ilivyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 7**.

**Jedwali Na. 7:** Kiwango cha Gharama za Uendeshaji: Tarakimu kwa Asilimia

| Description | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | 2026/27 |
|---|---|---|---|---|---|
| Gharama/Michango | 34.44 | 35.22 | 35.96 | 36.84 | 37.35 |
| Gharama/Mapato ya uwekezaji | 45.03 | 43.777 | 42.676 | 41.501 | 40.863 |
| Gharama/Jumla ya mapato | 19.50 | 19.50 | 19.50 | 19.50 | 19.50 |
| Gharama/Jumla ya rasilimali za Mfuko | 4.93 | 4.77 | 4.61 | 4.49 | 4.36 |

(h) Kwa kutumia makadirio ya mtathmini wa Mfuko, malipo ya fidia yanatarajiwa kufikia jumla ya Shilingi bilioni 44.79 ifikapo mwezi Juni 2027; na

(i) Idadi ya wafanyakazi wa Mfuko inatarajiwa kuwa 200 mwisho wa utekelezaji wa mpango huu. Ongezeko hili limesababishwa na kuimarishwa kwa ofisi za mkoa kufikia mwisho wa mpango huu. Jedwali Namba 8 linaonesha makisio ya wafanyakazi hadi kufikia mwisho wa mpango mkakati huu.

**Jedwali Na. 8:** Makisio ya Wafanyakazi kwa kipindi cha 2022/2023 hadi 2026/2027

| Year | Baseline 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | 2026/27 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya wafanyakazi | 135 | 148 | 160 | 170 | 180 | 190 |
| Ajira mpya | 13 | 12 | 10 | 10 | 10 | 10 |
| Jumla ya wafanyakazi | 148 | 160 | 170 | 180 | 190 | 200 |

## 4.3 Vyanzo vya Mapato

Vyanzo vikuu vya mapato ya Mfuko ni michango, mapato ya uwekezaji na mapato mengine yanayojumuisha riba na adhabu inayotokana na ucheleweshaji wa michango.

Katika kipindi tajwa, Mfuko unalenga kuongeza mapato kutoka Shilingi bilioni 155.95 kwa mwaka wa kwanza wa Mpango Mkakati hadi kufikia Shilingi bilioni 222.97 kwa mwaka wa mwisho wa utekelezaji wa Mpango Mkakati huu yaani 2026/27. Jedwali Namba 9 linaonesha makadirio ya mapato kutoka vyanzo mbalimbali.

## 4.4 Matumizi ya Mapato

Fedha zitakazokusanywa zinategemewa kutumika katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Mfuko kama yalivyoainishwa kwenye Sheria. Aidha, fedha husika zitatumika kulipa fidia, gharama za uendeshaji, kodi ya serikali, uwekezaji pamoja na matumizi mengine

ya maendeleo.

Katika kipindi tajwa, Mfuko utaendelea kudhibiti matumizi na kuhakikisha kuwa matumizi hayo hayazidi ukomo uliowekwa.

Kwa kutumia mikakati iliyowekwa, Mfuko utajikita katika kuboresha mafao kwa wanachama na kuimarisha uwezo wa Mfuko kifedha kupitia uwekezaji wenye tija na uboreshaji wa ukusanyaji wa michango.

## 4.5 Makadirio ya Kifedha

Jedwali Namba 9 na 10 yanaonesha makadirio ya kifedha kuanzia mwaka wa fedha 2022/23 hadi mwaka 2026/27 ambayo yameandaliwa kwa kutumia takwimu halisi hadi mwezi Juni 2021 na makadirio ya kufikia mwezi Juni 2027. Jedwali Namba 9 linaonesha taarifa ya mapato na matumizi na Jedwali Namba 10 linaonesha taarifa ya mizania.

**Jedwali Na. 9:** Taarifa ya Mapato na Matumizi (Kiasi kwa Shilingi Milioni)

| **Maelezo** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** | **2026** | **2027** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Kiasi tarajiwa** | | | | | |
| Michango ya waajiri | 82,376.92 | 88,299.18 | 94,638.61 | 101,415.66 | 108,667.84 | 116,397.54 |
| Mapato ya uwekezaji | 58,883.04 | 67,535.20 | 76,131.18 | 85,456.16 | 96,457.52 | 106,400.96 |
| Mapato mengine | 101.52 | 120.00 | 144.00 | 151.20 | 158.76 | 166.70 |
| **Jumla ya mapato** | **141,361.49** | **155,954.38** | **170,913.79** | **187,023.02** | **205,284.12** | **222,965.19** |
| **Matumizi** | | | | | | |
| Malipo ya fidia | 16,076.04 | 18,064.42 | 20,342.51 | 22,953.39 | 25,949.39 | 29,384.88 |
| Gharama za uendeshaji | 26,976.00 | 30,411.10 | 33,328.19 | 36,469.49 | 40,030.40 | 43,478.21 |
| Uchakavu wa rasilimali | 6,590.15 | 7,063.93 | 7,571.09 | 8,113.25 | 8,693.43 | 9,311.80 |
| Gharama za uwekezaji | 462.86 | 509.14 | 560.06 | 672.07 | 739.27 | 776.24 |
| Mchango wa Serikali | 1,500.00 | 1,500.00 | 1,500.00 | 1,500.00 | 1,500.00 | 1,500.00 |
| **Jumla ya matumizi** | **51,605.06** | **57,548.60** | **63,301.85** | **69,708.20** | **76,912.49** | **84,451.13** |
| | | | | | | |
| **Ziada kabla ya kodi** | **89,756.43** | **98,405.78** | **107,611.94** | **117,314.82** | **128,371.63** | **138,514.06** |
| | | | | | | |
| Kodi | 17,655.11 | 20,260.56 | 22,839.35 | 25,636.85 | 28,937.26 | 31,920.29 |
| | | | | | | |
| **Ziada ya mwaka** | **72,101.32** | **78,145.22** | **84,772.59** | **91,677.97** | **99,434.37** | **106,593.77** |

**Jedwali Na. 10:** Waraka Mizania (Kiasi kwa Shilingi Milioni)

| Description | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | 2026 | 2027 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Kiasi tarajiwa** | | | | | |
| Mali zisizohamishika mitambo na vifaa | 3,585.06 | 3,943.57 | 4,337.92 | 4,771.71 | 5,248.89 | 5,773.77 |
| Mali zisizoshikika | 2,088.11 | 1,879.30 | 1,691.37 | 1,522.23 | 1,370.01 | 1,233.01 |
| Uwekezaji | 499,054.20 | 577,606.82 | 658,910.86 | 748,867.35 | 846,540.21 | 949,589.86 |
| Mapato tarajiwa ya michango | 7,647.68 | 6,882.92 | 6,194.62 | 5,575.16 | 5,017.65 | 4,515.88 |
| Fedha taslimu | 2,488.96 | 2,240.06 | 1,892.55 | 2,044.79 | 1,850.25 | 1,418.55 |
| Rasilimali nyingine | 21,818.84 | 24,000.73 | 26,400.80 | 29,040.88 | 31,944.97 | 35,139.47 |
| **Jumla ya Rasilimali** | **536,682.85** | **616,553.38** | **699,428.12** | **791,822.13** | **891,971.97** | **997,670.53** |
| | | | | | | |
| **Madeni** | | | | | | |
| Malipo tarajiwa ya fidia | 8,143.56 | 8,957.92 | 8,062.12 | 8,868.34 | 8,690.97 | 8,777.88 |
| Malipo mengine | 9,109.62 | 10,020.58 | 9,018.52 | 8,928.33 | 9,821.17 | 8,839.05 |
| **Jumla ya madeni** | **17,253.18** | **18,978.49** | **17,080.64** | **17,796.67** | **18,512.14** | **17,616.93** |
| | | | | | | |
| **Jumla ya rasilimali halisi** | **519,429.68** | **597,574.89** | **682,347.48** | **774,025.46** | **873,459.83** | **980,053.60** |
| | | | | | | |
| **Fedha zilizolimbikizwa** | | | | | | |
| Rasilimali halisi mwanzoni mwa mwaka | 444,960.70 | 519,429.68 | 597,574.89 | 682,347.48 | 774,025.46 | 873,459.83 |
| Mapato kwa mwaka | 74,468.98 | 78,145.22 | 84,772.59 | 91,677.97 | 99,434.37 | 106,593.77 |
| **Jumla ya fedha zilizolimbikizwa** | **519,429.68** | **597,574.89** | **682,347.48** | **774,025.46** | **873,459.83** | **980,053.60** |

# SURA YA TANO

## 5.0 UFUATILIAJI WA MPANGO, TATHMINI NA UWAJIBIKAJI

### 5.1 Ufuatiliaji na Tathmini

Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango ni nguzo muhimu katika kuhakikisha malengo ya Mfuko yanafikiwa. Mpango mkakati wa Mfuko unatekelezwa kupitia mpango kazi wa kila mwaka unaoandaliwa kutoka katika malengo mkakati pamoja na shughuli mkakati. Katika kuhakikisha kuwa mpango kazi wa mwaka unatekelezwa, Mfuko utaandaa taarifa ya utekelezaji itakayotolewa kila mwezi, kila robo ya mwaka, kila nusu ya mwaka na kila mwaka.

Taarifa ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mpango mkakati itatumika kama njia mojawapo ya kuwezesha ufanyaji wa maamuzi. Kupitia mfumo wa kugawana, malengo mkakati ya Mfuko yatatoholewa na kukasimiwa kwa kurugenzi na idara za Mfuko ambao ndio watekelezaji wa shughuli mkakati. Aidha, mfumo wa usimamizi wa majukumu ya Mfuko utatumika kufanya tathmini ya utekelezaji wa shughuli mkakati katika ngazi za watumishi mara kwa mara.

#### 5.1.1 Uwajibikaji

Wadau mbalimbali watahusika kuhakikisha kuwa Mpango huu unatekelezwa kwa mafanikio. Mfumo wa tathmini na Ufuatiliaji wa Mfuko umeweka viashiria vikuu 25 vya ufikiaji wa malengo ambavyo vinaonesha utendaji wa Taasisi na idara zake. Vipimo vya viashiria ni mchanganyiko wa mahitaji, matokeo ya muda mfupi, matokeo ya muda wa kati, matokeo ya muda mrefu na athari.

Eneo kuu la msisitizo kwa Mfuko litakuwa ni kuratibu ufuatiliaji na tathmini . Hii inalenga kuboresha uwajibikaji na kuongeza ufanisi wa taasisi. Tathmini ya mara kwa mara na sahihi ya matokeo itakuwa moja ya njia za msingi za kuhakikisha mafanikio ya mpango mkakati. Utekelezaji wa Mpango utafanywa na Kurugenzi na vitengo vilivyooneshwa kwenye Muundo wa Mfuko kama unavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 1**.

#### 5.1.2 Kurugenzi inayohusika na Mipango

Kurugenzi inayohusika na Mipango itakuwa na jukumu la uratibu na uandaaji wa Mpango Mkakati, utekelezaji na ufuatiliaji na tathmini ya utendaji ili kuhakikisha kuwa mkakati unatoa matokeo yanayotarajiwa. Kurugenzi hiyo itasaidiwa na Timu ya Usimamizi ya kimkakati (SMT) ambayo itajumuisha wataalamu wenye ujuzi katika maeneo ya Mpango Mkakati, Ufuatiliaji na Tathmini, Usimamizi wa Mradi, Usimamizi wa Utendaji, Usimamizi wa Vihatarishi, TEHAMA, Fedha, Mabadiliko na Usimamizi wa Mawasiliano. Timu hii itahakikisha ufanisi katika uratibu wa utekelezaji na ufuatiliaji wa Mpango Mkakati. Katika kuhakikisha utekelezaji mzuri wa mkakati, Kurugenzi itafanya kazi kwa karibu na timu za mipango za idara.

### 5.1.3 Msimamizi wa Lengo

Menejimenti ya Mfuko itakuwa na jukumu la kusimamia utendaji wa jumla wa mpango mkakati wa Mfuko. Baadhi ya wajumbe wa Menejimenti wameteuliwa kama wasimamizi wa malengo ya kimkakati. Wasimamizi hawa watatoa ripoti za utekelezaji wa malengo mkakati na watakuwa na jukumu la kuunda mipango itakayotumika kutekeleza lengo mkakati na kupendekeza hatua za kurekebisha, pale inapobidi. Menejimenti ya Mfuko pia itapitia utekelezaji wa Mpango Mkakati na kufanya maamuzi ya kuboresha utekelezaji wa Mkakati.

### 5.1.4 Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani

Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kina jukumu la kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kutoa hakikisho juu ya utekelezaji wa Mpango Mkakati kwa Bodi na Menejimenti ya Mfuko.

### 5.1.5 Menejimenti

Menejimenti inawajibika kuandaa, kusimamia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango Mkakati.

### 5.1.6 Bodi ya Wadhamini

Bodi ya Wadhamini ndicho chombo cha juu cha usimamizi wa Mfuko. Katika kuhakikisha Mfuko unafikia malengo yake, Bodi ina jukumu la kupitia na kuidhinisha Mpango Mkakati, Mpango na Bajeti ya kila mwaka pamoja na kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkakati.

### 5.1.7 Mapitio ya Mpango Mkakati

Mpango huu utapitiwa baada ya nusu ya muda wa utekelezaji au wakati mwingine wowote ikihitajika kutokana na mabadiliko katika mazingira ya uendeshaji.




**Kielezo 1: MUUNDO WA TAASISI**

# Kiambatisho: MPANGO WA UTEKELEZAJI

## 1.0 LENGO: KUONGEZA KIWANGO CHA KURIDHIKA KWA WANACHAMA NA WADAU

**MMILIKI WA LENGO**: HHRMAU

| Shughuli Mkakati | Shabaha | Matokeo | | | | | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2022/23 | 2023/24 | 2024/2025 | 2025/26 | 2026/27 | |
| ♦ Kuandaa na kutekeleza Mpango Mkakati wa Utengema | Asilimia 80 ya ufanisi wa kiwango cha utengemao | ♦ Kuwahusisha watoa huduma za utengemao<br>♦ Jenga uwezo wa vituo vya kutolea huduma<br>♦ Ongeza wigo wa huduma za utengemao | ♦ Kuwahusisha watoa huduma za utengemao | ♦ Fanya marejeo na tekeleza Mkakati wa utengemao | ♦ Kuwahusisha watoa huduma za utengemao | ♦ Kuwahusisha watoa huduma za utengemao<br>♦ Anzisha kituo cha mfano cha huduma za utengemao | DAS |
| | ♦ Asilimia 80 ya wafanyakazi wapatiwe huduma za utengemao na kurejea kazini | ♦ Andaa na kutekeleza mpango mahususi wa ufuatiliaji wa<br>♦ Wahanga. | ♦ Andaa na kutekeleza mpango mahususi wa ufuatiliaji wa wahanga | ♦ Andaa na kutekeleza mpango mahususi wa ufuatiliaji wa wahanga | ♦ Andaa na kutekeleza mpango mahususi wa ufuatiliaji wa wahanga | ♦ Andaa na kutekeleza mpango mahususi wa ufuatiliaji wa wahanga | DAS |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ♦ Andaa na kutekeleza Mpango wa mawasiliano wa mabadiliko | ♦ Asilimia 90 ya wateja wana ufahamu juu ya Mfuko | ♦ Andaa maudhui ya kampeni ya uelimishaji<br>♦ Mkutano wa mwaka wa wadau umeandaliwa<br>♦ Angalau maadhimisho 4 yamehudhuriwa<br>♦ Programu 10 za uelimishaji zimefanyika<br>♦ Angalau Kampeni 4 za Kimkakati zimefanyika<br>♦ Fanya marejeo ya mkakati wa mawasiliano | ♦ Mkutano wa mwaka wa wadau umeandaliwa<br>♦ Angalau maadhimisho 4 yamehudhuriwa<br>♦ Programu 10 za uelimishaji zimefanyika<br>♦ Angalau Kampeni 4 za Kimkakati zimefanyika | ♦ Andaa maudhui ya kampeni ya uelimishaji<br>♦ Mkutano wa mwaka wa wadau umeandaliwa<br>♦ Angalau maadhimisho 4 yamehudhuriwa<br>♦ Programu 10 za uelimishaji zimefanyika<br>♦ Angalau Kampeni 4 za Kimkakati zimefanyika | ♦ Mkutano wa mwaka wa wadau umeandaliwa<br>♦ Angalau maadhimisho 4 yamehudhuriwa<br>♦ Programu 10 za uelimishaji zimefanyika<br>♦ Angalau Kampeni 4 za Kimkakati zimefanyika | ♦ Andaa maudhui ya kampeni ya uelimishaji<br>♦ Angalau maadhimisho 4 yamehudhuriwa<br>♦ Programu 10 za uelimishaji zimefanyika<br>♦ Angalau Kampeni 4 za Kimkakati zimefanyika | HPRU |
| | ♦ Fikia asilimia 90 ya ufanisi wa mawasiliano ya ndani | ♦ Andaa na kutekeleza mpango wa menejimenti ya mabadiliko | ♦ Tekeleza mpango wa menejimenti ya mabadiliko | ♦ Tekeleza mpango wa menejimenti ya mabadiliko | ♦ Tekeleza mpango wa menejimenti ya mabadiliko | ♦ Tekeleza mpango wa menejimenti ya mabadiliko | HPRU & HHRMAU |
| ♦ Andaa na kutekeleza Mpango wa menejimenti ya ubora wa huduma | ♦ Asilimia 90 kuridhika kwa wateja imefikiwa | ♦ Andaa na kutekeleza mwongozo wa menejimenti ya mahusiano na wateja, sera ya menejimenti ya malalamiko, mwongozo wa menejimenti ya malalamiko | ♦ Tekeleza mwongozo wa menejimenti ya mahusiano na wateja kwenye ngazi za idara | ♦ Tekeleza mwongozo wa menejimenti ya mahusiano na wateja kwenye ngazi za idara | ♦ Tekeleza mwongozo wa menejimenti ya mahusiano na wateja kwenye ngazi za idara | ♦ Tekeleza mwongozo wa menejimenti ya mahusiano na wateja kwenye ngazi za idara | |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | ♦ Sera ya Uwajibikaji wa Shirika kwa Jamii imepitiwa<br>♦ Viwango vya ISO vimejumuishwa kwenye mfumo wa utendaji kazi<br>♦ Tathmini na ufuatiliaji wa utendaji wa taasisi na miradi imefanyika | ♦ Fanya tafiti kuhusu menejimenti ya mahusiano na wateja<br>♦ Mwongozo wa upigaji chapa umepitiwa<br>♦ Asilimia 80 ya zana za kujitangaza zimebuniwa na kuzalishwa<br>♦ Ofisi 2 za Mfuko zimewekewa chapa za utambulisho<br>♦ Tuzo 3 za nje zimepatikana<br>♦ Sera ya Uwajibikaji wa Shirika kwa Jamii imetekelezwa<br>♦ Wadau 8 muhimu wamepewa udhamini<br>♦ Viwango vya ISO vimejumuishwa kwenye mfumo wa utendaji kazi<br>♦ Tathmini na ufuatiliaji wa utendaji wa taasisi na miradi imefanyika | ♦ Fanya tafiti kuhusu menejimenti ya mahusiano na wateja<br>♦ Mwongozo wa upigaji chapa umepitiwa<br>♦ Asilimia 80 ya vifaa vya kujitangaza vimebuniwa na kuzalishwa<br>♦ Ofisi 2 za Mfuko zimewekewa chapa za utambulisho<br>♦ Tuzo 3 za nje zimepatikana<br>♦ Sera ya Uwajibikaji wa Shirika kwa Jamii imetekelezwa<br>♦ Wadau 8 muhimu wamepewa udhamini<br>♦ Viwango vya ISO vimejumuishwa kwenye mfumo wa utendaji kazi<br>♦ Tathmini na ufuatiliaji wa utendaji wa taasisi na miradi imefanyika | ♦ Fanya tafiti kuhusu menejimenti ya mahusiano na wateja<br>♦ Mwongozo wa upigaji chapa umepitiwa<br>♦ Asilimia 80 ya zana za kujitangaza zimebuniwa na kuzalishwa<br>♦ Ofisi 2 za Mfuko zimewekewa chapa za utambulisho<br>♦ Tuzo 3 za nje zimepatikana<br>♦ Sera ya Uwajibikaji wa Shirika kwa Jamii imetekelezwa<br>♦ Wadau 8 muhimu wamepewa udhamini<br>♦ Viwango vya ISO vimejumuishwa kwenye mfumo wa utendaji kazi<br>♦ Tathmini na ufuatiliaji wa utendaji wa taasisi na miradi imefanyika | ♦ Fanya tafiti kuhusu menejimenti ya mahusiano na wateja<br>♦ Mwongozo wa upigaji chapa umepitiwa<br>♦ Asilimia 80 ya zana za kujitangaza zimebuniwa na kuzalishwa<br>♦ Ofisi 2 za Mfuko zimewekewa chapa za utambulisho<br>♦ Tuzo 3 za nje zimepatikana<br>♦ Sera ya Uwajibikaji wa Shirika kwa Jamii imetekelezwa<br>♦ Wadau 8 muhimu wamepewa udhamini<br>♦ Viwango vya ISO vimejumuishwa kwenye mfumo wa utendaji kazi<br>♦ Tathmini na ufuatiliaji wa utendaji wa taasisi na miradi imefanyika | HPRU |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | ♦ Asilimia 90 ya imani ya wadau kwa Mfuko imefikiwa | ♦ Andaa na kutekeleza programu ya kushirikisha wadau | ♦ Andaa na kutekeleza programu ya kushirikisha wadau | ♦ Andaa na kutekeleza programu ya kushirikisha wadau | ♦ Andaa na kutekeleza programu ya kushirikisha wadau | ♦ Andaa na kutekeleza programu ya kushirikisha wadau | DO |

## 2.0 LENGO: IMARISHA UWEZO ENDELEVU WA KIFEDHA

**MMILIKI WA LENGO: DFPI**

| Shughuli Mkakati | Shabaha | Matokeo | | | | | Mhusika |
